




**Wawili** wauawa na tembo wakijipiga 'Selfie' UK. 2




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Septemba 2, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581421

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Samia aanika siri panguapangua ya mawaziri

UKURASA 2





Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimpongeza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, baada ya kuapishwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Ikulu Ndogo Zanzibar jana. Wanaoshuhudia ni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango. **PICHA: OWM**


## Matatani tuhuma kuua mkwe kisa kutolipa mahari

UKURASA 7

**RIPOTI MAALUM**

# Anayedaiwa kunajisi mwanawe atoroka akiwa mahabusu Polisi

• **KAMANDA** asema choo kilitumika kulaghai askari *Ukurasa 4*




**MICHEZO** **SIMBA SC YAONGEZA DOZI** UK.24 **MAONI** UK.6

HABARI KITAIFA

## Wauawa na kundi la tembo wakitaka kupiga nao picha

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

KUNDI la tembo saba waliokuwa wanaswagwa na maofisa wanyamapori kwa kushirikiana na jeshi la polisi wilayani Hanan'g mkoani Manyara, wamevamia Kijiji cha Mreru na kuwaua watu wawili na kujeruhi wengine wawili.

Akizungumza na Nipashe jana, Kkamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP) George Katabazi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi majira ya saa 10:30 jioni.

Kamanda Katabazi aliwataja waliouwawa kuwa ni Emmanuel Florian (33) mkazi wa Hydom na Daniel Marko (20) mkazi wa Dumbeta. Aliwataja majeruhi kuwa ni Anna Michael (40) mkazi wa Dumbeta na Emmanuel aliyefahamika kwa jina moja na wote wamelazwa katika wako Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara wakipatiwa matibabu.

Katabazi alisema chanzo cha tukio hilo ni kundi la tembo saba waliokuwa wanaswagwa na maofisa wanyamapori kutoka kwenye makazi ya watu kwenda katika Hifadhi ya Misitu ya Dirma.

Alisema waliofariki dunia walikanyagwa na tembo hao eneo la tukio huku ikidaiwa kuwa Emmanuel alitaka kupiga picha wanyama hao huku Daniel akiwa amemshika mkia tembo mmoja kati ya wale saba.

Kuhusu mama aliyejeruhiwa, Kamanda alisema alivunjwa miguu yote miwili na alikutwa nyumbani kwake. Katabazi alisema ni vizuri wananchi wakiona wanyama wakali wasiwasogelee na kama wanataka kupiga picha wawasiliane na mamlaka zinazohusika na wanyama.

Vilevile alisema wananchi wakiona wanyama wakali watoe taarifa mapema ili mamlaka husika ziwasaidie na wanaoishi maeneo ya shoroba au mapito ya wanyama waondoke na ikiwezekana wazungumze na mamlaka ziwaonyeshe mipaka sahihi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Catherine Magali akizungumza kwa njia ya simu na Nipashe, alikiri kuwapokea wagonjwa hao na hali zao zinaendelea vizuri.

# Samia aanika siri panguapangua mawaziri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema mabadiliko aliyoyafanya katika Baraza la Mawaziri si adhabu bali yanalenga kuimarisha utendaji kazi huku akiwataka wateule hao kutambua kuwa ni watumishi wa watu.

Aliyasema hayo katika hafla ya kuwaapisha viongozi aliowateua hivi karibuni wakiwamo mawaziri, manaibu waziri, makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu, iliyofanyika Ikulu Ndogo, Zanzibar iliyoko Tunguu mkoa wa Kusini Unguja.

Dk. Samia alisema katika utumishi wa watu, uhusiano ni jambo zuri, hivyo wakijiona wako juu kwa kuwa wamepata uteuzi, hawatowatumikia watu na hatimaye kuleta mabadiliko katika utendaji kazi.

Kutokana na hali hiyo, Rais Samia aliwataka viongozi hao kuwa wapole na kabla ya kutoa uamuzi ni lazima kufikiria jambo na kutulia.

"Sasa ukijipandisha unataka kukaribia mbinguni kuwa umepata uteuzi wa kujionyesha wewe ni nani hutotumikia watu. Upole si ujinga bali ni maarifa," alisema.

Samia alisema anahitaji mabadiliko ya yale yote waliyowaahidi wananchi katika kuleta maendeleo, hivyo wateule hao wanapaswa kuwa na uhusiano mzuri katika kuwatumikia watu. "Twendeni tukabadilike, tukasimamie utendaji na kutekeleza yale yote yaliyowekwa ili kupata maendeleo mazuri zaidi," alisema.Kuhusu aliyemteua kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema mwakani kuna kivumbi hivyo ana hakika anaweza kukabiliana nacho na kumsisitiza kupiga kazi.

"Mengine sitaki kuyachambua, wanasema usimwage mtama kwenye ndege wengi. Sasa mtama wetu tutauchambua ndani katika kikao kazi ambacho kitafanyika muda mfupi baada ya hafla hii," alisema.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema mabadiliko hayo ni sawa na timu ya mpira ambapo kocha hufanya mabadiliko ya namba za wachezaji na baraza hilo la mawaziri sura ni zile zile ila wamebadilishiwa wizara tu.

Aliwataka viongozi hao kuleta tija zaidi katika utendaji, hivyo kufanya kazi wa ushirikiano na watendaji wanaowaongoza na kuzingatia falsafa ya kiongozi mkuu ya kusimamia mabadiliko katika eneo lake. Dk. Mpango alisema ni muhimu kuwa na masikio ya kusikiliza kero za wananchi Bara na Visiwani na kuzifanyia kazi kwa sababu kuna baadhi ya maeneo kelele ni kubwa ikiwamo migogoro ya ardhi.

Alisema pia upande wa maliasili, ugomvi uliopo kati ya wananchi na hifadhi ni mkubwa, hivyo kushirikiana na Waziri wa Mifugo (na Uvuvi) katika kutatua.

"Mheshimiwa Rais ameona ni vyema apange safu ambayo itafunga magoli zaidi ili twende kuanzia mwaka kesho, uchaguzi wa serikali za mitaa hadi uchaguzi mkuu kufunga magoli ya uhakika na si ya kubabaisha,"alisema.

Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, aliwahakikishia ushirikiano viongozi hao walioapishwa ili kudumisha na kuendeleza Muungano wa Tanzania.

"Naridhika sana na mambo mengi ya ushirikiano yanayofanyika kati ya serikali ya Muungano na ya Zanzibar ambayo si ya Muungano na ya Muungano. Ningependa tuendeleze utamaduni wetu huu kwa maslahi ya pande mbili zote za muungano" alisema Dk Mwinyi.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, dini na viongozi wa vyama vya siasa.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Prof. Said Aboud (wa pili kushoto), akiangalia majani yanayotumika kama tiba kwa magonjwa mbalimbali huku akisikiliza maelezo kutoka kwa Mtunza Hazina wa Shirikisho la Vyama vya Tiba asili Tanzania, Dk. Zena Haukalaga 'Mama Masai' (kulia), alipotembelea wiki ya tiba asili ya mwafrika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Kaimu Meneja wa NIMR Mabibo, Emmanuel Peter na Mkurugenzi Msaidizi Kitengo cha Tiba Asili na Tiba Mbadala Wizara ya Afya, Dk. Liggyle Vumilia. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Askari polisi aliyeua aachiwa huru

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Morogoro imemwachia huru askari polisi Koplo Mapalala (36) wa Kituo cha Polisi Mvuha mkoani hapa baada ya kuonekana hana hatia katika kesi ya mauaji bila kukusudia alipokuwa akitimiza wajibu wake kazini.

Akizungumza wakati akisoma hukumu, Jaji wa Mahakama hiyo, Messe Cheba, alisema mahakama imemwachia mshtakiwa chini ya kifungu namba 38 kifungu kidogo cha kwanza cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022 baada ya kuonekana hana hatia.

Jaji Cheba alisema mahakama katika kutoa hukumu hiyo, imezingatia kuwa mshtakiwa hana historia ya makosa ya kijinai na pia ni mkosaji wa mara ya kwanza huku akiwa anatimiza wajibu wake kazini sambamba na kulinda upotevu wa silaha kwa mujibu wa kanuni za kijeshi.

Mawakili wa Jamhuri, Jumanne Milanzi na Edna Aloyce, walidai mahakamani hapo kuwa siku ya tukio mshtakiwa akiwa na askari mwenzake Koplo Patrice, walikwenda kumkamata mtu aliyetuhumiwa kufanya uharibifu wa makusudi kwenye mali za kijiji.

Ilidaiwa wakati wa ukamataji, mshtakiwa na mwenzie hawakuwahi kumkamata mtuhumiwa bali mtu huyo akiwa na wenzake, waliwazunguka huku wakiwa na silaha mbalimbali za jadi wakimtishia kumpiga.

Katika juhudi za kutaka kuwatawanya wananchi hao waliowazunguka, Mapalala alifyatua risasi moja hewani lakini bado wananchi hao, akiwamo marehemu, waliendelea kuwatishia kuwapiga na silaha ndipo mshtakiwa alimfyatulia risasi eneo la mguuni na kupelekwa Hospitali ya Wilaya iliyoko Mvuha na walipofika madaktari walisema alikuwa amefariki dunia kwa kupoteza uhai akiwa njiani.

Ilidaiwa kuwa uchunguzi ulifanyika na kuonyesha kifo hicho kilisababishwa na kutokwa na damu nyingi kulikotokana na kuvunjika kwa mshipa wa mguu wa kulia.

Wakili Jumanne Milanzi aliiomba mahakama kumpa adhabu stahiki mshtakiwa kwa mujibu wa sheria kwa sababu hana mamlaka ya kutoa uhai wa mtu bali ni Mungu pekee ndiye mwenye mamlaka hiyo.

Pia alidai kuwa kitendo alichofanya ni cha kinyama na kosa kisheria.

Aidha, Wakili Milanzi alida kuwa kulingana na ushahidi uliotolewa mahakamani, mshtakiwa ni askari wa polisi ambaye ana mafunzo na anaelewa namna ya kutumia silaha sambamba na kuzingatia mazingira ya ukamataji, hivyo alipaswa kujiandaa lakini alishindwa na kusababisha matumizi mabaya ya silaha na kusababisha kifo.

Wakili wa utetezi, Fredy Sanga, aliiomba mahakama inapotafakari adhabu stahiki ya kumpatia mteja wake, itoe adhabu yenye huruma kwa sababu mshtakiwa kama alingekuwa na lengo la kufanya mauaji angetekeleza kwa kuwa alikuwa na silaha aina ya AK 47 ikiwa na risasi 30 huku akiwa amezungukwa na kundi la watu wenye hasira.

Sanga pia alidai kuwa mshtakiwa alitambua kufanya mauaji ni kosa kwa mujibu wa sheria ndiyo maana alimpiga marehemu risasi ya mguuni ili kutuliza ghasia hizo na kufanikisha ukamataji wake.

# Jela miaka saba kujifanya mganga, kuua

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MAHAKAMA Kuu kanda ya Morogoro, imemhukumu kifungo cha miaka saba jela Jumanne Ngalaba (28) mkazi wa Kisaki, baada ya kukiri kosa la kumuua mke wa mwanajeshi bila kukusudia.

Akitoa hukumu hiyo jana, Jaji wa Mahakama hiyo, Messe Chaba, alisema mahakama imempa adhabu hiyo kwa mujibu wa sehemu ya 198 ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022 ili iwe fundisho kwake na kwa wenzake.

Jaji Chaba alisema katika kutoa hukumu hiyo mahakama imezingatia maombolezo ya upande wa utetezi kwamba mshtakiwa alikiri kutenda kosa na kutosumbua mahakama huku akiwa amekaa mahabusu miaka mitatu sambamba na kifungu hicho cha sheria kinachosema adhabu ni miongoni mwa kuachiwa huru au kufungwa maisha ambapo mshtakiwa hakupaswa kufungwa maisha sababu alikiri kosa.

Akisoma maelezo ya kosa, Wakili wa Serikali, Jumanne Milanzi, alidai kuwa siku ya tukio, Christina Ndimbati ambaye kwa sasa ni marehemu, alikuwa na wageni wawili mmoja akiwa mganga wa kienyeji ambaye ndiye mshtakiwa na kuendelea kumpatia matibabu. Baadaye, mgeni mwingine aliondoka na kubaki Ngalaba kisha ikabainika kuwa Ndimbati alitoweka na mshtakiwa pia alitoweka.

Alidai kuwa baada ya wote kutoweka, shemeji wa Ndimbati aliamua kumtafuta ndugu yake bila mafanikio huku simu yake ikiita bila kupokelewa lakini baadaye ilizimwa kabisa ndipo aliamua kutoa taarifa serikali ya mtaa na polisi.

Wakili Milanzi alidai mshtakiwa alikamatwa akiwa amevalia sare za jeshi la kujenga Taifa (JWTZ) katikati ya stendi ya mabasi mkoani Tabora na alipohojiwa alikiri kusababisha kifo cha marehemu wakati akimpatia matibabu na baadae aliamua kuondoka na sare hizo ambazo ni mali ya mume wa marehemu.

Wakili huyo alidai mshtakiwa aliongoza askari polisi hadi kwenye eneo la Maseyu alipofukia mwili wa marehemu ambao ulifukuliwa na uchunguzi wa kidaktari uligundua kuwa chanzo cha kifo cha mwanamke huyo kilisababishwa na kukosa hewa kulikosababishwa na kukabwa.

Aidha, Wakili Milanzi aliiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu stahiki kwa mujibu wa sheria kwa sababu hakuna mwenye mamlaka ya kuondoa uhai wa mtu zaidi ya Mungu mwenyewe na kwamba Ndimbati alikuwa mama wa familia ambaye ameacha watoto watatu waliokuwa wanamtegemea baada ya kuondokewa na baba yao.

Pia wakili huyo alidai Ndimbati alikuwa na wazazi waliokuwa wakimtegemea katika misaada licha ya kuwa tegemezi na nguvu kazi kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Wakili wa utetezi, Jobit Byaragaba, aliiomba mahakama kumpa adhabu yenye huruma mshtakiwa kwa kuzingatia ni mkosaji wa mara ya kwanza na amekaa gerezani zaidi ya miaka mitatu, hivyo amejifunza na anajutia makosa yake.

Pia wakili huyo alidai kuwa mshtakiwa ana wazazi wanaomtegemea na pia ana watoto watatu ambao baada ya tukio hilo, mama yao aliwakimbia, hivyo hawako kwenye mikono salama ya malezi zaidi ya mshtakiwa kama mlezi wao mkuu.

Akisoma maelezo ya awali, Msaidizi wa Kumbukumbu wa Mahakama, Justa George, alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo Mei 24, 2020 katika eneo la Kayenzi, Kata ya Mafisa kwa kumuua Ndimbati bila kukusudia.



Baadhi ya wafugaji jamii ya kimasai wa kijiji cha Maharaka, kata ya Boma, wilayani Mvomero mkoani Morogoro, wakiangalia ng'ombe wa wafugaji wenzao, waliolala chini na kushindwa kutembea baada ya kukatwa na mapanga na kundi la watu wasiojulikana wakati wakinyweshwa maji katika Mto Maharaka jana. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Ng'ombe wa mil. 20/- wakatwa mapanga, mchungaji ajeruhiwa

**Na Ashton Balaigwa,** MVOMERO

NG'OMBE 13 wenye thamani ya Sh. milioni 20, mali ya wafugaji wa jamii ya Kimasai katika Kijiji cha Maharaka, Mvomero mkoani Morogoro, wamekatwakatwa na mapanga na mmoja wa wafugaji kujeruhiwa na kikundi cha watu ambao mpaka sasa hawajajulikana.

Mmoja wa wamiliki wa ng'ombe hizo, Mbayani Kipereni, mkazi wa Doma, alisema tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 6:30 mchana pembezoni mwa Mto Maharaka walipokwenda kunywesha maji ng'ombe hao na gafla wakavamiwa na kundi la watu.

Alisema baada ya kuvamiwa, kundi hilo lilianza kuwashambulia na kuwajeruhi wakiwa na mapanga na silaha mbalimbali huku wengine wakiwakatakata kwa mapanga ng'ombe hao na wakikimbia na mpaka sasa hawajulikani waliko.

'Tulikuwa tunapeleka ng'ombe katika eneo la kunyweshea ambako ni Mto Maharaka na hakuna eneo lolote la shamba lenye mto. Ghafla tulivamiwa na kundi kubwa la watu wakaanza kutupiga na wengine kukata ng'ombe mapanga," alisema Kipereni.

Mmliki mwingine wa ng'ombe hao, Adam Nduli, alisema wanashangaa kuvamiwa na kundi hilo wakati eneo hilo la mto kwa miaka mingi wamekuwa wakitumia kunyweshea mifugo yao.

Alisema wanashangazwa na kitendo kilochofanywa na kundi hilo kwa kuwa hakuna shamba lolote ambalo mpaka sasa limeharibiwa na mifugo, hivyo kuiomba Serikali kuingilia kati ili kuepusha kutokea kwa athari zingine.

Naye mmoja wa wafugaji kutoka Kata ya Doma, Kisonga Kipareni, alisema tatizo hilo limekuwa likichangiwa na baadhi ya viongozi wa kata ambao hakuwataja vyeo wala majina, kwa kuwazuia wafugaji kunywesha mifugo yao katika mto Maharaka wakati hakuna sehemu nyingine yenye maji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi (ACP) Alex Mkama, alikiri kuwepo kwa tukio hilo alilosema limefanywa na kundi la wahalifu ambao mpaka sasa hawajulikani.

Mkama alisema kundi hilo liliwavamia wafugaji hao na kukatakata ng'ombe kwa mapanga na kumjeruhi mmoja wa wafugaji kati ya wawili waliokuwa wakinywesha mifugo yao.

Alisema mpaka jana mchana, ng'ombe 13 walikuwa wamekatwakatwa mapanga na tayari jeshi hilo limeanza msako dhidi ya waliofanya tukio hilo na kuendelea kuimarisha ulinzi katika eneo hilo.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
02.09.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumanne tarehe 05-09-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero** kupitia Mikumi, gari hiyo ina namba ya usajili:
**T 204 DYJ / T 887 DJB T 792 DYL /T 879 EAU**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
**Urefu** - **mita 22.00**
**Upana** - **mita 4.20**
**Kimo** - **mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero** kupitia **Mikumi,** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

RIPOTI MAALUM

# Anayedaiwa kumbaka mwanawe atoroka akiwa mahabusu ya Polisi

**Na Halfani Chusi**

BABA anadaiwa kunajisi mwanawe kwa miaka mitatu mfululizo. Ni simulizi ngumu kuaminika na yenye utata, lakini polisi wanadai amewatoroka akiwa katika mahabusu yao.

Ni mwezi mmoja sasa tangu kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo, Daniel Simle, katika makazi yake kijijini Ilewelo, kata ya Manzase, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma.

Simle anadaiwa kufanya ukatili huo kwa miaka mitatu, tangu mwaka 2021, dhidi ya mwanawe mwenye umri wa miaka tisa sasa. Alikamatwa na polisi Julai 30 mwaka huu na kuwekwa mahabusu katika Kituo cha Polisi Mvumi, wilayani Chamwino, lakini akadaiwa kuwatoroka polisi siku mbili baadaye.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi Martin Otieno, akitoa ufafanuzi kwa mwandishi wa habari hizi kuhusu tukio hilo, alisema:

"Ni kweli kesi hiyo ninaifahamu. Mtuhumiwa alitoroka akiwa mikononi mwetu. Alimlaghai (askari) polisi kwamba anataka kwenda kujisaidia haja ndogo walipokaribia kwenye choo, alichoropoka na kutimua mbio, askari aliyekuwa naye akazidiwa.

"Taratibu za kumkamata baada ya kutoroka chini ya ulinzi zinaendelea. Jalada la kutoroka limefunguliwa, tunamtafuta kwa kutumia njia ya mtandao na muda siyo mrefu tutamkamata ili afikishwe katika vyombo vya sheria, akapambane na kesi yake ya kubaka (kunajisi) mtoto wake wa miaka tisa.

"Nina uhakika atapatikana! Nimeshatoa maelekezo atafutwe kwa njia yoyote. Hivi ni vitendo ambavyo havikubaliki na havivumiliki. Sijui watu wanakuwa na imani za kishirikina au nini... ni kitu ambacho hakiingii akilini kwa mtu mwenye akili timamu kufanya ukatili kama huo."

**MAMA ALONGA**

Mama wa mtoto huyo, Sukaina... (jina la pili tunalihifadhi) anasema kwamba, wakati ukatili huo unafanywa, mwanawe huyo wa kike alikuwa anaishi na baba yake wilayani Chamwino, yeye alikuwa Tabata jijini Dar e Salaam. Alivunja ndoa na mumewe mwaka 2019.

"Kabla ya kuvunja ndoa miaka mitano iliyopita, tulikuwa tunaishi pamoja hapa Dar es Salaam, maeneo ya Tabata Kisukulu, baada ya hapo, yeye (mtuhumiwa) akahamia Dodoma.

"Nilizaa naye mtoto mmoja, ambaye ndiye huyo aliyembaka (aliyemnajisi). Tulipokuwa tunavunja ndoa nilitaka kuishi na mwanangu, lakini alilazimisha akae naye yeye. Ilifika hatua ananitishia hadi kuniua, kumbe lengo lake lilikuwa kumbadili awe mke wake," analalama.

Mama huyo (37), anasema kuwa Agosti Mosi mwaka huu, akiwa Dar es Salaam, alipigiwa simu na mwanamke aliyejitambulisha kwake ni mama wa kambo wa mwanawe, akimpatia taarifa za ukatili huo. Alishtuka.

Hatua alizochukua, mama huyo anasema alipiga simu kwa shemeji yake, anayeishi Chamwino, akamwezesha kuongea na mwanawe kujua ukweli wa taarifa alizopewa kisha kuhitaji kupata namba za simu za Ofisa Mtendaji wa Kijiji ili achukue hatua za awali wakati anajipanga kwenda huko.

"Shemeji anamwogopa kaka yake, akashindwa kumpeleka mtoto kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji. Ikabidi mwanangu aende peke yake kutoa maelezo na kumpatia namba yangu ya simu. Alipotoa maelezo, mtendaji akampeleka hospitalini ili akapimwe kama kweli amefanyiwa ukatili huo.

"Baada ya kupewa majibu na daktari kama mtoto amefanyiwa ukatili huo, alinipigia simu akanieleza hali ilivyokuwa. Nikamwomba ahakikishe mtuhumiwa huyo anakamatwa, apelekwe polisi, mimi ninakuja huko kwa ajili ya kuendesha kesi hiyo.

"Ndipo mtendaji huyo akachukua jukumu la kutoa taarifa Kituo cha Polisi Mvumi, ilipofika jioni siku hiyo (Julai 30 mwaka huu), alinitaarifu kama tayari mtuhumiwa ameshakamatwa na yuko kituo cha polisi," alisema.

Sukaina anasema kuwa Agosti Mosi mwaka huu, alifunga safari kwenda Chamwino.

Alifika usiku na pasi na kupoteza muda, aliamua kwenda moja kwa moja hadi Kituo cha Polisi Mvumi, alikomtaarifu Mkuu wa Kituo kuwa alikwenda huko kwa ajili ya taratibu za kisheria.

"Kwa sababu ilikuwa usiku, ikabidi niende kulala nyumba ya wageni. Kulipokucha asubuhi (Agosti 2 mwaka huu), nilikwenda tena Kituo cha Polisi alikokuwa anashikiliwa mtuhumiwa. Nilimkuta Mkuu wa Kituo, akaniambia mtuhumiwa ametoroka jana jioni (Agosti Mosi mwaka huu)," anadai.

Sukaina, kama alivyosimuliwa baadaye, anadai mtuhumiwa majira ya 11 jioni aliwalaghai askari waliokuwa zamu kwamba alitaka kwenda hajandogo na akatumia mwanya huo kutoroka.

Anabainisha kuwa kutokana na mtuhumiwa kutoroka katika mazingira hayo, siku iliyofuata polisi walimchukua mtoto kwa mama wa kambo na kumwamuru aondoke naye. Kamanda Otieno alithibitisha askari wake kuchukua hatua hiyo kwa ajili ya usalama wa mtoto.

Mama huyo anadai kuwa tangu alipoondoka Chamwino na kurejea Dar es Salaam akiwa na mwanawe huyo aliyekuwa anasoma darasa la nne, amekosa ushirikiano toka kwa Jeshi la Polisi anapohoji kama limemkamata mtuhumiwa.

"Ninaomba mwanangu asaidiwe apate uhamisho wa shule haraka ili niendelee kukaa naye mwenyewe huku Dar es Salaam kwa ajili ya usalama wake, Mtuhumiwa hajulikani aliko, anaweza akamvizia hata njiani akamteka kupoteza ushahidi.

"Na pia yuko darasa la nne, anahitaji kufanya Mtihani wa Taifa wa Darasa la IV mwezi wa 10 (Oktoba) na hapa alipo ameshakosa mtihani wa majaribio kwa sababu amesajiliwa shule ya huko Dodoma yalikomfika makubwa. Na anahitaji kwenda kufanya Mtihani wa Taifa hukohuko na mimi uwezo sina na kipato changu kidogo," analalama mama huyo aliyetawaliwa na simanzi huku akimweleza mwandishi hisia zake dhidi ya anachokiita 'mchezo mchafu' uliosababisha mtuhumiwa kutoroka.

**MAMA WA KAMBO**

Janeth Luminu, mama wa kambo aliyekuwa anaishi na mtoto huyo, anasema kuna kipindi aliposafiri na kumwacha mtoto huyo na baba yake nyumbani, aliporejea aliona mabadiliko katika mwili wake.

"Unamkuta mtoto amekonda. Unapomwuliza 'kwanini umekonda? Niliposafiri uliumwa?' Ananiambaia 'hapana, sikuumwa!' Kumbe kuna kitu kilikuwa kinaendelea, aliogopa kuniambia.

"Kujiokoa, pale (mtoto) alipoona mambo yanamzidia, akaenda kumweleza baba yake mdogo na kumwomba amwelekeze kwa Mtendaji wa Kijiji alikotoa maelezo ya kile anachofanyiwa na baba yake.

"Nilikuwa sijui, nikaona ghafla askari wamemkamata baba yake. Mtoto aliporudi kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji, nikamwuliza 'kwani vipi, mbona wamemkamata baba yako?'

"Akanijibu 'mimi huwa ninaogopa kukwambia, maana (baba) alisema nikikwambia wewe, atanichinja anitumbukize kwenye karo la choo. Sasa nimeona nimwambie bamdogo (baba mdogo) aombe namba za simu za mama na anielekeze kwa mtendaji ili nipate msaada'," Janeth anasimulia.

Mama huyo anasema alishangaa kuona mumewe baada ya kukamatwa na polisi, hakukaa muda mrefu mahabusu, akaachiwa. Alipotoka alikwenda kumtapeli jirani yao ambaye ni mfanyabiashara. Alipopewa fedha (Sh. milioni 2.1), hakurejea nyumbani. Baadaye wakapata taarifa alikuwa amewatoroka polisi.

Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya, alipotafutwa na mwandishi kuzungumzia tukio hilo, alisema mama wa mtoto (Sukaina) alishafika ofisini kwake kulalamika kuhusu mtuhumiwa kutoroka polisi.

Msuya alisema kuwa alipohitaji taarifa za tukio hilo toka kwa Ofisa Upelelezi wa Polisi Wilaya, mrejesho ni kwamba, mtuhumiwa alifikishwa mahakamani, taarifa ambazo zinakinzana na kauli ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi Otieno.

**DAKTARI AFUNGUKA**

Mkuu wa Idara ya Ukunga Hospitali ya Mvumi (DCT), Mwate Tungaraza, anasema kuwa baada ya kumfanyia uchunguzi mtoto huyo, walibaini kutendwa ukatili huo. Alikuwa na michubuko, pia walikuta mbegu za kiume sehemu za siri.

"Nilipompima, nilibaini kweli alikuwa amebakwa na alikuwa na ... (alitaja neno lenye maana ya mbegu za kiume). Alikuwa ametoka kuingiliwa muda siyo mrefu. Pia, maumbile yake yalikuwa yametanuka na hata nilipomnusa, nilikuta ana harufu ya mtu aliyetoka kufanya mapenzi," Dk. Mwate anafafanua.

Tabibu huyo anasema kuwa wakati anamtibu, mtoto huyo alimwambia amekuwa anafanyiwa ukatili huo na baba kwa miaka mitata sasa.

Hii ina maana kwamba mtoto huyo mwenye umri wa miaka tisa kwa sasa, alianza kufanyiwa ukatili huo akiwa na umri wa miaka sita, akiwa mwanafunzi wa darasa la kwanza.

"Huyo mtoto ameharibiwa sana. Anahitaji ushauri nasaha. Kwa jinsi alivyokuwa anaelezea maumbile ya baba yake na alivyokuwa anamwingilia, anamjua kiundani baba yake," tabibu huyo anasema, akiwa na mshangao mtuhumiwa kutoroka akiwa mahabusu ya polisi.

Dk. Mwate anabainisha kuwa ofisini kwake kwa mwaka huu pekee, tayari ameshapokea kesi nne za watoto kunajisiwa, akishauri elimu itolewe kwa jamii kwa kuwa udadisi wao umebaini wengi wanaotenda matukio hayo wana imani za kishirikina.

**ITAENDELEA KESHO.**



Mama wa mtoto akisimulia mkasa wa mwanawe.

# Bilioni 460/- kukusanywa kutimiza masharti kupata msaada wa GPE

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kukusanya Sh. bilioni 465 kupitia wadau wa sekta ya elimu nchini kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji msaada wa Sh. bilioni 125.2 kutoka shirika linaloundwa na Mataifa yenye Uchumi mkubwa duniani (G7) Global Partnership for Education (GPE).

Lengo ni kusaidia nchi zenye uchumi wa chini zilizoathirika na vita na magonjwa.

Katika hafla ya kutambua mchango wa wadau wa sekta ya elimu jijini Dar es Salaam juzi, Mwenyekiti wa GPE, Rais mstaafu wa awamu ya nne Jakaya Kikwete, alisema ni muhimi kila aliyetoa ahadi akatimiza, ili kuhakikisha nchi inapata fedha hizo kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya elimu.

Alisema mchango huo utawezesha serikali kupata msaada kutoka shirika hilo kwa kigezo cha multiplier grand, yaani kuwa na mtaji kwanza ili kupata sifa za kupatiwa fungu toka shirika hilo.

"Sh. bilioni 465 zimewasilishwa na wakuu wa mikoa kwa niaba ya wadau wa elimu ambazo wamechangia kwa lengo la kuiwezesha serikali kupata msaada wa Sh. bilioni 125.2 kutoka GPE, ili kuwekeza katika miradi mipya ya elimu nchini," alifafanua Kikwete.

Alisema kuwa serikali mshirika wa GPE, kwanza hutakiwa kuwashawishi wadau wengine kuwekeza kama wafadhili wenza katika miradi mipya ya elimu kwa njia ya mkopo au misaada ndipo GPE itoe fedha ya miradi.

Alibainisha kuwa kila dola moja itakayopatikana kupitia ufadhili kutoka sekta binafsi kama vile asasi za kiraia, benki au kampuni, GPE nayo itatoa dola moja. Unachangiwa kulingana na ulichotoa.

Mwenyekiti huyo alisema kwa kila dola tatu itakayosamehewa kutoka katika taasisi za kimataifa au nchi washirika wa maendeleo na kuwekezwa sekta ya elimu, GPE itatoa dola moja.

Kikwete pia alimshauri Waziri ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kuwekeza katika masomo ya sayansi, akisisitiza hakuna maendeleo ya nchi bila uwekezaji katika sekta ya elimu, hasa masomo hayo.

"Kila mwaka kwenye matokeo ya kidato cha nne, somo la Hisabati haliridhishi na sisi kama wadau wa elimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - UDSM (Kikwete ni Mkuu wa chuo hicho) tutakaa na kujadili, ili tujue shida ipo kwetu sisi tunaofundisha walimu vyuoni au ipo wapi," alisema.

Waziri wa Elimu, Prof. Mkenda, alisema: "Hakuna maendeleo yoyote katika nchi bila elimu na tusipowekeza katika sekta hii, watu wengine watakuja kutusaidia kuendesha shughuli zetu na ndiyo maana serikali inawekeza zaidi."

Waziri huyo pia aligusia mchakato wa kuboresha elimu, akiutaja ni njia ya kuboresha mifumo ya elimu nchini badala ya kuwa na mitaala mipya kila wakati ambayo haitofanyiwa kazi na itakuwa katika karatasi na ndio maana wanaendelea na maboresho ya sekta hiyo kupitia mtaala wa mwaka 2014.

Katika hafla hiyo, Kikwete alitoa tuzo kwa wakuu wa mikoa kutambua mchango wao katika kuimarisha sekta ya elimu nchini.

***Imeandaliwa na Emmaloveness Mkanula na Mwanahamisi Mussa (TUDARCo)**

# Wafanyakazi 166 Ngorongoro walipwa mafao

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) imepokea mafao ya Bima ya Group Endowment Assurance Scheme (GEAS) kwa watumishi wake 166.

Wafanyakazi hao ni waliokuwa wamekata bima ya mfuko wa maisha inayotoa mafao kwa wafanyakazi wake wanapostaafu au kufariki.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka NCAA, watumishi hao walikata bima kupitia kampuni ya ushauri wa bima ya Intertrade Express Limited ambayo ni wakala wa Shirika la Bima la Taifa (NIC).

Taarifa hiyo ilisema malipo ya mafao ya awamu ya kwanza yalifanyika Desemba, mwaka jana, awamu ya pili Machi na ya tatu Agosti, mwaka huu.

Malipo hayo ni matokeo ya utekelezaji wa maagizo ya Kamshina wa Bima Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware, kulipa wanufaika wote wa skimu ya bima ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Wafanyakazi hao wamelipwa kwa mujibu wa mkataba na makubaliano ya pande zote yaliyofanyika Juni 9, 2022.

Baada ya kupokea malalamiko kutoka NCAA, Kamishna wa Bima aliunda kamati maalum iliyojumuisha wajumbe kutoka TIRA, Ngorongoro, NIC na Intertrade ambao wote ni wahusika katika suala hilo.

NCAA imetoa shukrani za dhati kwa TIRA kwa ushirikiano ilioutoa katika kuhakikisha watumishi hao wanalipwa mafao ya GEAS.

Taarifa hiyo ilisema TIRA ikiwa ni mamlaka ya usimamizi wa sekta ya bima, itaendelea kuhakikisha haki za wanufaika wa bima mbalimbali zinalindwa na kupatikana kwa wakati.

Taarifa hiyo iliwataka watanzania kuendelea kutumia huduma za bima nchini na kutosita kuwasilisha malalamiko yao kwa Kamishna wa Bima pindi wanapoona kampuni za bima haziwatendei haki. Ilisema Kamishna wa Bima amepewa mamlaka kupitia Sheria ya Bima SURA Na. 394, kutoa adhabu kwa mtu yeyote, Kampuni au taasisi itakayobainika kuvunja Sheria ya Bima.


The Guardian Limited

## JOB VACANCY

The Guardian Limited, **Publishers of leading Tanzanian newspapers, The Guardian, Nipashe and Nipashe Jumapili, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

### SENIOR MARKETING EXECUTIVE – DAR ES SALAAM

**Job Purpose:**

Developing and executing strategies to promote brands, products and services, maximizing profits for the company.

**Main Responsibilities:**

- Formulate an appropriate commercial strategy that responds to the overall development of the company's marketing operations, newspaper sales, advertisements and other printed products.
- Become knowledgeable expert of The Guardian Limited products and be experienced in identifying target markets and developing strategies to communicate with them.
- Identify, plan, prepare and produce proposals for the targeted audiences.
- Study competitors' products and services on a daily basis, with a view to designing counter strategies.
- Advise clients on their advertising and promotion campaigns.
- Organize all company events related to CSR, promotion, product launching, staff parties, etc.
- Monitor and analyze product performances, trends and provide accurate reports on programe and market information.
- Explore ways of improving existing products and services and increasing profitability.
- Advise the Management with feasibility studies on ways to get sponsorship for various events, highlighting benefits to the Company.
- Engage in negotiating and closing deals where and if appropriate.
- Prepare periodic performance reports for the Management and provide appropriate inputs towards improvement and the taking of remedial measures.
- Design and implement human resources training and development programme

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 5 years' relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge and familiarity with a wide range of newspaper brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via email address: vacancy@guardian.co.tz by **8th September, 2023.**

**NB:** Only shortlisted candidates will be contacted.

***Please note that The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dirisa la usajili limefungwa, sasa kazi kwenu wachezaji

**USAJILI** wa wachezaji watakaoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, First League, Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania na Ligi Kuu Zanzibar kwa msimu wa mwaka 2023/2024 ulifungwa rasmi juzi usiku.

Pia tarehe hiyo ilikuwa ni mwisho wa usajili wa mashindano ya kimataifa yanayofanyika kila mwaka ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Katika mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ni timu tatu tu zimebakia katika kupeperusha bendera ya Tanzania ambazo ni Yanga, Simba zote za Dar es Salaam na Singida Fountain Gate FC kutoka mkoani Singida.

Kumalizika kwa mchakato huo wa usajili, ni ishara kila timu sasa iko tayari kuanza mapambano ya kufikia malengo yake iliyojiwekea katika msimu huu.

Ni jambo ambalo liko wazi katika ligi hizo zote hapa nchini ambazo zinasimamiwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), timu zimejigawa katika makundi matatu.

Kuna kundi la kwanza ambalo wakati linafanya usajili wake na maandalizi ya Pre Season, lenyewe linalenga kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na Kombe la FA, huku wale wanaoshiriki michuano ya kuwania Ngao ya Jamii, wakijipanga pia kushinda taji hilo ili kuuanza vyema na kwa furaha msimu mpya.

Kundi la pili ni lile lenye timu ambazo tangu kuanza kwa msimu zinasema malengo yao ni kumaliza katika nafasi nne za juu ili kujihakikishia tiketi ya kushiriki kwenye mashindano ya kimataifa na waliobakia wao tangu kuanza kwa ligi huonekana wakipambana kusaka idadi ya pointi zitakazowanusuru na janga la kushuka daraja.

Hili si la kujifisha, linajulikana na hii imetokana na baadhi ya timu misimu yote kuzoeleka zinasindikiza wenzake na huchagua za kupambana kusaka ushindi au angalau kuondoka na pointi moja huku zikidharau michezo mingine na mwisho wa siku huangukia katika kushuka daraja moja kwa moja au kunusurika kwenye michezo ya 'Play Off'.

Wakati timu zikitakiwa kubadilika na kufikiria kutwaa taji la ligi husika, huu ni wakati muhimu kwa wachezaji wote waliopata nafasi ya kusajiliwa kujituma na kuonyesha ubora wao ambao uliwavutia makocha kuwasajili katika vikosi vyao.

Kila mchezaji anayepata nafasi ya kucheza anatakiwa kujituma na kuisadia timu yake kufikia malengo kwa sababu ndio sababu kuu iliamua kumsajili yeye na kuwaacha nyota wengine, watumie vyema nafasi wanazopata ili kunadi zaidi vipaji vyao.

Tayari kila timu inayoshiriki Ligi Kuu Bara imeshacheza mechi mbili, kuna wachezaji waliopata nafasi ya kupangwa katika kikosi cha kwanza na walioingia wakitokea benchi, kila mmoja kwa wakati wake anatakiwa kutumia muda huu wa mapumziko ya kupisha kalenda ya kimataifa kujitathmini na baadaye kurejea wakiwa imara.


Kwa wachezaji ambao hawajapata nafasi ukiondoa wale majeruhi, huu ni wakati wa kurekebisha mapungufu yenu na kuwashawishi makocha kuwajumuisha katika 'First Eleven' mara michezo ya Ligi Kuu itakaporejea pamoja na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Nyota ambao wanatarajia kushiriki Ligi ya Championship, First League, Ligi Kuu ya Wanawake na Ligi Kuu Zanzibar, bado hamjachelewa, endeleeni kujituma na kuonyesha bidii katika mazoezi na hatimaye mtakuwa sehemu ya wachezaji tegemeo wa timu.

Kila mchezaji anatakiwa awe na malengo, na ili kufikia malengo, ni lazima kujituma na kuwa na nidhamu ya mchezo ndani na nje ya uwanja. Wachezaji kutohofia majina ya wachezaji wakubwa wa wanaojiita wakongwe kwa sababu wao pia waliwahi kuwa chipukizi, wakati wa kufanya mabadiliko ni huu kwa kila mmoja kupambana kwa lengo la kupata namba ya kudumu katika timu yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Simba, Yanga zitavuna mabao, makocha wasipobadili mifumo

Na Adam Fungamwango

**IWAPO** makocha wa timu nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu Bara wasipobadili mifumo na kung'ang'ania kupaki basi wanapocheza dhidi ya Simba na Yanga, huenda tukaendelea kushuhudia klabu hizo kongwe msimu huu zikishindana kufunga mabao mengi kila wanaposhuka dimbani kusaka pointi tatu muhimu.

Nimeshuhudia mechi mbili za Simba na Yanga ambazo zimechezwa kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, Simba ilishinda mabao 4-2 katika mechi iliyofanyika kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani Morogoro na ule iliocheza kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam dhidi ya Dodoma Jiji ilishinda mabao 2-0.

Lakini ukiiangalia mechi ile ni wachezaji wenyewe wa Simba walikuwa wanakosa mabao, laiti kama wangetulia wangeweza kupachika au kuondoka na ushindi wa magoli matano mpaka nane.

Yanga katika mechi mbili imefunga jumla ya mabao 10, ikiitungua KMC magoli 5-0 na kipigo kama hicho ikakutana nacho JKT Tanzania ambaye imerejea tena katika Ligi Kuu.

Ukiangalia timu zote hizo ni makocha wao wanatengeneza mfumo wa kuzuia zaidi kuliko kushambulia.

Zinazuia zaidi ili zishambulie kwa kushtukiza. Nilivyoziangalia mechi zote ni timu iliyoweza kuucheza mfumo huo ni Mtibwa Sugar peke yake.

Ni kwa sababu walikuwa na wachezaji wenye uwezo wa kukimbia. Unapocheza mfumo wa 'kupaki' basi ni lazima uwe na wachezaji wakimbiaji zaidi ambao wanaweza kutoka eneo moja hadi jingine kwa kasi na kwa muda mfupi, lakini pia kuwa na straika mmoja mwenye nguvu ya kukabiliana na mabeki wawili kwa wakati mmoja akiwa peke yake.

Pamoja na kufungwa lakini Mtibwa Sugar ilionekana ndio timu pekee iliyoweza kuucheza mfumo huo wakiongozwa na straika wao, Matheo Antony, aliyefunga mabao mawili kwenye mechi hiyo.

Lakini timu zingine hazikuuweza kabisa mfumo huo, badala yake zilikuwa zikikaa tu nyuma bila hata kujua wafanye nini wakiupata mpira.

Hawakuwa na watu wa kukimbia na kutoka haraka nyuma kwenda mbele, badala yake wakawa wanapasiana hapo hapo nyuma bila malengo mpaka wananyang'anywa na kusababisha tena hatari nyingine kabla ya kufungwa.

Unapocheza na Simba au Yanga, halafu wachezaji wa timu pinzani wakawa wakiupata mpira hawana cha kufanya wanapasiana tu pasi fupi fupi nyuma, tegemea kuruhusu bao pale unaponyang'anywa mpira.

Nilichogundua makocha wanatengeneza mfumo wa kupaki basi wanawafanya wachezaji wao kuzuia sana kipindi cha kwanza na hatimaye wanachoka kipindi cha pili na kuruhusu mabao mengi.

Sipingi mfumo huo, lakini makocha waangalie kama wana aina ya wachezaji wanaoweza kuendana na mfumo huo.

Kama huna straika mwenye nguvu mbele, na wachezaji wenye mbio ni kazi bure. Ni afadhali tu kucheza kwa kupishana kuliko kuzuia kwa muda mrefu halafu timu inafungwa mabao mengi kwa dakika chache kutokana na wachezaji kuchoka.

Ukiangalia hata ligi mbalimbali Ulaya, timu ikipaki basi, ujue ina aina hiyo ya wachezaji na wakifanya shambulizi la kushtukiza inakuwa hatari.

Kwenye mechi za Ligi Kuu nimeshuhudia timu inapaki basi na wala haishambulii kabisa dakika zote.

Ni ngumu sana kupata bao katika hali hii, na cha kujiuliza hizi timu zinapocheza na timu hizi kubwa huwa zinahitaji ushindi au sare?

Inawezekana kabisa wakati mwingine timu hizi kubwa hazipotezi mechi kwa sababu hazishambuliwi sana.

Kwa usajili mkubwa uliofanywa na timu mbalimbali msimu huu, pamoja na ubora wa ligi yetu, ni vyema kwa makocha wakatengeneza mifumo rafiki itakayowasaidia kulingana na vikosi vyao badala ya kutumia asilimia zaidi ya 90 wanapocheza na vigogo hawa kupaki basi, wakati wa kubadilika ni huu kabla mambo hayajaharibika sana.

## Mbaroni tuhuma kula njama kumuua mkwe

**Na Christina Haule,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linawashikilia watu sita kwa tuhuma za mauaji, wakiwamo ndugu wanaodaiwa kula njama na kumuua mkwe wao, Hassan Ngema (51) - mkazi wa Itegete, wilayani Morogoro kwa madai ya kushindwa kulipa mahari.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama, tukio hilo lilitendwa Agosti 28 mwaka huu saa 11:30 jioni huko Itegete, wilaya na Mkoa wa Morogoro.

Kamanda Mkama aliwataja wanaoshikiliwa kuwa Masele Machibya Masele (65) - mkazi wa Tabora ambaye ni baba mkwe wa marehemu, Mwalu Hassan (18) na Pawa Kema (16) - watoto wa marehemu na Rehema Masele (35) ambaye ni mke wa marehemu, wote wakiwa ni wakazi wa Kitongoji cha Itegete, wilayani hapa.

Alisema watuhumiwa hao, kwa pamoja, walikula njama - mtuhumiwa namba moja (Masele) ni baba mkwe wa marehemu ambaye alitoka mkoani Tabora kwenda kudai mahari.

"Baada ya kuona ameshakaa muda mrefu na mwanawe na kuzaa naye watoto wawili bila kulipa mahari na anakuwa mkaidi, ndipo wakala njama na kumuua," alisema.

Kamanda huyo alisema uchunguzi wa tukio hilo unaendelea. Watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

Katika tukio lingine, watoto wawili wenye umri wa miaka 15 kila mmoja (majina tunayahifadhi), wote wakazi wa Kata ya Kidugalo, wanashikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma za kumuua kwa kumpiga virungu na fimbo sehemu mbalimbali za mwili, Habibu Dakawa (26), mkazi wa Ngerengere.

Kamanda huyo alisema watuhumiwa hao walitenda kosa hilo Agosti 28 mwaka huu na kwamba aliyeuawa alikuwa anazuia mifugo waliyokuwa wanachunga isiingie katika shamba lake la mikorosho.

Pia alisema wanawashikilia watu 102 kwa tuhuma za kukamatwa na kilogramu 508.6 za dawa za kulevya aina ya bangi na kilo mbili za mirungi katika maeneo mbalimbali ya mkoani hapo.



Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kampala cha Gongo la Mboto, Neema Mpigiye akizungumza kuhusu umuhimu wa wazazi kupeleka watoto shule, ili wapate elimu kwa wakazi wa Kata ya Kipunguni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wadau 3,300 kushiriki Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika 2023

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema zaidi ya watu 3,300 wamejiandikisha kuhudhuria Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika, litakalofanyika Dar es Salaam kwa mara ya kwanza na kuleta pamoja wakuu wa nchi watano.

Waziri wa Maendeleo Norway, mawaziri 30 wa nchi tofauti za Afrika, wakuu wa taasisi zaidi ya 500 pia wameahidi kuhudhuria mkutano huo ambao unaleta pamoja wataalamu, watafiti, wakulima, wafugaji na wavuvi katika kutatua changamoto na kuwa na mwelekeo wa pamoja.

Hayo yalibainishwa juzi jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, wakati wa mdahalo wa waandishi wa habari na taasisi za fedha nchini ulioandaliwa na Media Brain kuelekea Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika linalotarajiwa kufanyika Septemba 5 hadi 8 mwaka huu.

Alisema msimamo wa serikali ni kuwawezesha wakulima kumudu gharama za uzalishaji na wataendelea kuhakikisha wanawawekea mazingira mazuri, ili wafanye kilimo biashara na kujikwamua kiuchumi.

"Mipango yetu kwa sasa tunawaangalia wakulima wadogo, hata sera zetu ni kuhakikisha tunaongeza tija na kuwapatia mazingira mazuri katika kufanya shughuli zao za kilimo.

"Mpaka sasa tumesajili vijana 150 wanajishughulisha na kilimo, mifugo na mazao ya chakula watakaohudhuria mkutano huu. Hii yote inaonesha ni kwa namna gani serikali inawajali vijana hawa," alisema Mweli.

Alisema Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika 2023 litakuwa na maeneo matatu ambayo ni maandalizi, mkutano wenyewe pamoja na kuangalia namna ya utekelezaji wa maazimio yatakayotolewa.

"Tumefanikiwa kupata watu wengi ukilinganisha na mwaka jana lilivyofanyika Kigali, Rwanda walihudhuria watu 2,000. Hii ni kutokana na utashi wa Rais Samia Suluhu Hassan na namna ambavyo tumejipanga katika kuwashirikisha watu mbalimbali kushiriki wakiwamo wafanyabiashara, wakulima wenyewe pamoja na wawekezaji, " alisema.

Alisema kutakuwa na chumba maalum kwa wawekezaji wa nje ya nchi na ndani ambao watajadiliana katika biashara, utafiti na kubadilishana ujuzi.

Meneja Mwandamizi wa Kilimo Biashara wa CRDB, Maregesi Shabani, alisema zaidi ya Sh. trilioni 1.3 zimeelekezwa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. Wanawafikia wazalishaji kuanzia ngazi ya chini hadi taifa.

Mkuu wa Ushauri wa Kilimo Biashara wa NMB, Issac Msasu, alisema wametoa zaidi ya Sh. trilioni 1.6 kwa sekta hiyo kwa lengo la kubadilisha maisha yao na kuhakikisha upatikanaji chakula nchini.

Mkuu wa Kilimo Biashara wa NBC, Raymond Urassa, alisema benki hiyo ipo tayari kuwasaidia wakulima na matazamio yao makubwa ni kuwawezesha watu hao kiuchumi na kiteknolojia.

Meneja Mwandamizi Kilimo Biashara wa Equity, Teofira Madilu, alisema wameweka malengo ya kuwafikia kundi la wakulima, wafugaji na wavuvi milioni 25 na mwaka jana walitoa zaidi ya Sh. bilioni 50 huku mwaka huu hadi Juni wakitoa zaidi ya Sh. trilioni 2.5.

Kaimu Mkurugenzi wa Sera, Utafiti na Mipango wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Waziri Mkani, alisema mifumo ya uzalishaji ni changamoto kubwa kwa wakulima, mifugo na uvuvi na kwamba benki hiyo imekuwa ikitoa mikopo kwa kundi hilo katika kuongeza uzalishaji.

# Mbunge alia uhaba nyumba za polisi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, amehoji mpango wa serikali wa kujenga nyumba za askari polisi ikiwamo Wilaya ya Ikungi kutokana na wengi wao kupanga nyumba mitaani.

Akiuliza maswali jana bungeni, Mtaturu alisema kuna uhaba mkubwa wa makazi ya askari katika wilaya hiyo na kwamba hakuna nyumba na hata mkuu wa polisi wa wilaya analazimika kupanga nyumba mtaani.

Pia alihoji lini serikali itajenga vituo vya polisi kwenye kata za Mkiwa, Misughaa na Mungaa kwenye jimbo hilo kutokana na ukuaji wa kiuchumi unaongeza matatizo ya kiusalama kwenye maeneo mbalimbali.

"Tulikubaliana kuwa na polisi kata, sasa polisi kata bila kituo ni sawa na bure. Nini mkakati wa serikali wa kujenga vituo hivi hasa kata za pembezoni ili kusaidia ulinzi. Tayari wananchi wamefyatua matofali katika kata ya Mkiwa 1000 na kupitia mfuko wa jimbo na mimi nimeanza kuwaunga mkono, je nini serikali itafanya kusaidia kukamilisha ujenzi huu?" alihoji. Akijibu maswali hayo kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema moja ya mikakati ya serikali ni kuimarisha ulinzi na usalama kwa kuhakikisha askari wanaishi maeneo stahiki karibu na maeneo ya kazi na kupitia bajeti zake itaendelea kutenga fedha kwa ajili hiyo.

Aidha, alisema serikali ina taarifa kuwa kata za Mkiwa, Misughaa na Mungaa zimeshatenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Polisi na nyumba za makazi ya askari. "Serikali kupitia Jeshi la Polisi inasubiri kupata taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa vituo na nyumba hizo ili kuunga mkono kwenye ukamilishaji," alisema.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Maida Hamad Abdallah, alihoji lini serikali italipa madeni ya fedha za kusafirishia mizigo kwa askari wastaafu.

Akijibu swali hilo, Kigahe alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi imefanya uhakiki wa madeni ya kusafirisha mizigo ya askari polisi wastaafu 624.

"Uhakiki huo unaonesha kuwa jumla ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya kusafirisha mizigo ya askari polisi wastaafu ni Sh. milioni 806.06. madai hayo yatalipwa baada ya Wizara ya Fedha kukamilisha taratibu za kuhamishia fedha hizo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kukamilishwa,"alisema.

# Ardhi yaja na mabadiliko makubwa kimfumo

**Na Munir Shemweta,** BAGAMOYO

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imesema inaendelea kufanya maboresho makubwa ya kimfumo na muundo kwa lengo la kuwezesha mambo mengi kufanyika kimfumo.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhandisi Anthony Sanga, alisema hayo juzi wakati akizindua mpango wa kuondoa mlundikano wa mashauri katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, mjini hapa.

Sanga alisema kumekuwa na tatizo kubwa hasa wananchi wa kawaida wanapokwenda ofisi za ardhi kupata namba ya malipo (control number), hivyo wizara inakuja na mfumo utakaomwezesha mwananchi kupata namba hiyo bila usumbufu.

"Kumekuwa na changamoto kubwa hasa wananchi wetu wa kawaida wanapokwenda ofisi zetu za ardhi kupata tu 'control number'. Suala hili limekuwa kama sehemu ya watu kujinufaisha sasa tunakuja na mfumo utakaomwezesha mwananchi kupata namba hiyo mwenyewe," alisema.

Kwa mujibu wa sanga, hata suala la kufanya uchunguzi kwa wananchi wanaotaka kununua nyumba au kiwanja nalo anaweza kufanya mwenyewe wakati kwa sasa analazimika kutoa fedha ili kufanyiwa.

"Mnafahamu mtu akitaka kununua nyumba au kiwanja cha mtu katika kufanya upekuzi anaambiwa pia alipe Sh. 40,000 au 100,000 afanyiwe haraka haraka. Nayo pia tunaenda kukomesha. Mwananchi atafanya upekuzi mwenyewe," alisema.

Mhandisi Sanga aliongeza kuwa katika maboresho hayo ni suala la kulipia kodi ya pango la ardhi na kazi hiyo itakamilika hivi karibuni kwa wananchi kulipia kupitia simu za mkononi sambamba na kupata bili kama wanavyopata kwenye maji.

"Utakapokuwa na namba ya NIDA utapata mambo yote, katika wizara yetu ya ardhi wamelizingatia agizo la Mhe. Rais ambapo kwa kutumia kitambulisho cha NIDA mwananchi atapata taarifa zote kuhusiana na masuala ya ardhi" alisema Mhandisi Sanga.

Akigeukia suala la kuondoa mlundikano wa mashauri ya ardhi, alisema uzinduzi huo umefanyika pia kwenye wilaya za Musoma, Tarime, Kilombero na Tabora katika kipindi cha mwezi mmoja na kwamba mashauri 500 yanatarajiwa kusikilizwa na kutolewa uamuzi.

"Katika kipindi takriban siku nane toka kuanza kwa zoezi hili, wenyeviti wamesikiliza mashauri 243 katika mabaraza niliyoyataja, na kazi hii inaendelea," alisema.

Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba za Wilaya nchini, Stela Tullo, aliishukuru wizara kupitia Mradi wa Uboreshaji Miliki za Ardhi kwa kuyawezesha mabaraza kuhakikisha yale yanayoelemewa na migogoro angalau yanapata msaada wa wenyeviti kwenda kwenye mabaraza yenye mashauri mengi na kuyakalia vikao maalum kwa lengo la kusikilizwa na kutolewa maamuzi kwa wakati na haki.



Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu akizungumza bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge alia uhaba nyumba za polisi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, amehoji mpango wa serikali wa kujenga nyumba za askari polisi ikiwamo Wilaya ya Ikungi kutokana na wengi wao kupanga nyumba mitaani.

Akiuliza maswali jana bungeni, Mtaturu alisema kuna uhaba mkubwa wa makazi ya askari katika wilaya hiyo na kwamba hakuna nyumba na hata mkuu wa polisi wa wilaya analazimika kupanga nyumba mtaani.

Pia alihoji lini serikali itajenga vituo vya polisi kwenye kata za Mkiwa, Misughaa na Mungaa kwenye jimbo hilo kutokana na ukuaji wa kiuchumi unaongeza matatizo ya kiusalama kwenye maeneo mbalimbali.

"Tulikubaliana kuwa na polisi kata, sasa polisi kata bila kituo ni sawa na bure. Nini mkakati wa serikali wa kujenga vituo hivi hasa kata za pembezoni ili kusaidia ulinzi. Tayari wananchi wamefyatua matofali katika kata ya Mkiwa 1000 na kupitia mfuko wa jimbo na mimi nimeanza kuwaunga mkono, je nini serikali itafanya kusaidia kukamilisha ujenzi huu?" alihoji.

Akijibu maswali hayo kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema moja ya mikakati ya serikali ni kuimarisha ulinzi na usalama kwa kuhakikisha askari wanaishi maeneo stahiki karibu na maeneo ya kazi na kupitia bajeti zake itaendelea kutenga fedha kwa ajili hiyo.

Aidha, alisema serikali ina taarifa kuwa kata za Mkiwa, Misughaa na Mungaa zimeshatenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Polisi na nyumba za makazi ya askari.

"Serikali kupitia Jeshi la Polisi inasubiri kupata taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa vituo na nyumba hizo ili kuunga mkono kwenye ukamilishaji," alisema.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Maida Hamad Abdallah, alihoji lini serikali italipa madeni ya fedha za kusafirishia mizigo kwa askari wastaafu.

Akijibu swali hilo, Kigahe alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi imefanya uhakiki wa madeni ya kusafirisha mizigo ya askari polisi wastaafu 624.

"Uhakiki huo unaonesha kuwa jumla ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya kusafirisha mizigo ya askari polisi wastaafu ni Sh. milioni 806.06. madai hayo yatalipwa baada ya Wizara ya Fedha kukamil-

# 'Acheni kuwaficha wagonjwa fistula'

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI ya CCBRT imewataka watanzania wasiwafiche wanawake wanaougua ugonjwa wa fistula kwani ugonjwa huo unatibika na wengi waliotibiwa hospitalini hapo wamepona.

Mganga Mkuu wa Hospitali hiyo, Dk. Cyprian Tomoka, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari waliotembelea hospitali hiyo kujionea shughuli mbalimbali.

Alisema kwa mwaka hospitali hiyo imekuwa ikifanya upasuaji wa wastani wa wagonjwa kati ya 400 na 600 na ambao wamekuwa wakipona ugonjwa huo kabisa na kuendelea na maisha yao ya kawaida ikiwemo kupata watoto

"Kwa bahati mbaya sana wagonjwa hawa wanafichwa huko maeneo ya vijijini, wanatelekezwa na waume zao na ndugu zao wanapopata ugonjwa huu lakini niwaambie kwamba unatibika kabisa," alisema

"Sisi tuna mtandao wetu wa nchi nzima wanaokusanya watu wa aina hiyo kwa hiyo kama kuna mtu anamjua mwanamke mwenye shida ya kutokwa na mkojo bila kuudhibiti awasiliane na watu wetu wamlete," alisema

Dk. Tomoka alisema mwanamke anapoona dalili za kushindwa kuzuia haja ndogo au haja kubwa baada ya kujifungua ni vizuri akamuona mtaalamu wa afya na kufanyiwa uchunguzi ili kuthibitisha kama ana fistula ya uzazi.

Alitaja moja ya dalili za fistula ya uzazi kuwa ni kutokuwa na uwezo wa kuzuia haja ndogo au kubwa au kwa pamoja baada ya kujifungua na kuongeza kuwa fistula ya uzazi haitokani na kulogwa, laana wala kutembea na wanaume wengi wakati wa ujauzito kama inavyovumishwa mitaani.

Alisema mama mjamzito anapaswa kuhudhuria kliniki mara kwa mara ili kupima maendeleo ya ujauzito wake na kupata ushauri hali ambayo inaweza kusaidia kwa kiwango kikubwa asipate matatizo hayo wakati atakapojifungua.

Alisema mbali na CCBRT hospitali zingine zinazotibu fistula ya uzazi ni Martenity Africa Hospital ya Kivulini Arusha, Bugando Mwanza na Nkinga Tabora.



## Wananchi watakiwa kuchukua tahadhari mvua El-Nino

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imezielekeza kamati za usimamizi wa maafa nchini kushirikiana na umma kuchukua tahadhari ya madhara ya mvua za El-Nino inayotarajiwa kunyesha mwisho wa mwaka huu na kuendelea.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama alitoa agizo hilo wakati alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa, jana.

Mhagama alizitaka kamati za kusimamia maafa na sekta nchini kushirikiana na umma kuchukua tahadhari za madhara ya mvua hizo.

Alisema tahadhari hiyo ya serikali inatokana taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini (TMA), iliyotolewa Agosti 24, mwaka huu kuwa utabiri wa mwelekeo wa mvua za msimu wa vuli kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Desemba, mwaka huu na kuendelea Januari, 2024 kuwa unaonyesha uwapo wa El-Nino.

Aliyataja madhara yanayoweza kutokea ni mafuriko kuharibu miundombinu, madhara ya kiafya, kiuchumi, kijamii na upotevu wa mali.

Alitaja madhara mengine kuwa ni maporomoko ya ardhi kuathiri makazi, mazingira, mashamba, usafiri na shughuli zingine za uchimbaji madini.

Pia, mlipuko wa magonjwa ya binadamu, wanyama na wadudu waharibifu wa mazao na mimea.

Kadhalika alizitaka kamati hizo kutambua maeneo hatarishi na yenye viashiria vya kuathirika na maafa na kuandaa mipango ya kuzuia madhara na maafa endapo yatatokea.

Alizitaka kuainisha na kuandaa rasilimali za usimamizi wa maafa kwa kila sekta kushiriki kikamilifu katika eneo lake pamoja na kuandaa mipango ya kuzuia milipuko ya magonjwa ya binadamu na wanyama.

Waziri Mhagama alisema tahadhari zingine zinazotakiwa kuchukuliwa na umma ni kuhifadhi mazingira na kulinda miundombinu ya barabara, maji umeme na mawasiliano ili kupatikana na huduma wakati wowote endapo mvua hizo zitanyesha.

Pia, alizitaka kamati hizo kuelimisha wananchi hatua za kuchukua tahadhari ili kuokoa maisha na mali pamoja na kutoa taarifa za haraka kwa mamlaka husika kuhusu dalili za kutokea au yanapotokea maafa.

Alisema mikoa inayohusishwa zaidi ni inayopata mvua mara mbili katika msimu ambayo ni Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, kusini mwa Mkoa wa Simiyu, kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma, Dar es Salaam, Tanga, Pwani na Mkoa wa Morogoro.

Alitoa wito kwa wananchi kutumia mvua hizo vizuri ili ziwe na manufaa kupitia shughuli za uzalishaji mali kama kilimo, kuandaa mabwawa na malambo kwa ajili ya kuvuna maji.

Alisema kuwa maji hayo yanaweza kutumika kupanda mazao yanayohitaji maji mengi kama vile mpunga, uzalishaji samaki na kuandaa na kuhifadhi malisho ya mifugo.

# Wanao okota vyuma chakavu mitaani wahadharishwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania (TAEC), Prof. Lazaro Busagala, amewaonya watu wanaojihusisha na shughuli za uokotaji vyuma chakavu mitaani kuacha mara moja.

Alisema hali hiyo itawasaidia kujiepusha na madhara ya kiafya wanayoweza kuyapata kutokana na baadhi ya vyuma vilivyopo mitaani ambavyo vimekuwa vikiingia nchini kuwa na viasili vya mionzi hatari.

Prof. Busagala, alisema hayo juzi jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara ya Balozi wa Tanzania nchini Austria Naimi Aziz, kutembelea makao makuu ya Tume hiyo nchini.

"Nitowe wito kwa wananchi ambao wamekuwa wakijihusisha na shughuli za uokotaji wa vyuma chakavu kuacha mara moja kwani vinaweza kuwa na viasili vya mionzi mikali ambayo inaweza kuwasababishia madhara kiafya," alisema. Alisema siyo jambo sahihi kiafya kwa wananchi kuendelea kuokota vyuma chakavu mitaani bila Tume hiyo kuvifanyia vipimo kama vina viasili vya mionzi hatari kwa afya zao.

"Historia inaonyesha kuwa mataifa mengi yamepata hasara mtu anaweza kuokota chuma chenye viasili vya mionzi ambacho kikatumika kwenda kutengenezea nondo ambazo zikatumika kujengea majengo mionzi ile itakwenda kuathiri watu wengi," alisema Prof. Busagala.

Aidha, aliwataka wananchi kuitumia Tume hiyo kupima maji ili kubaini kama ni salama kwa matumizi ya binadamu.

"Tume hii ni mtambuka inaingia katika sekta mbalimbali kwenye maji, kilimo, afya hivyo ni lazima itumike kupima vitu kama maji ili kuhakikisha kuwa afya za wananchi zinakuwa salama na maji wanayotumia kuthibitishwa kuwa hayana viasili vya mionzi," alisisitiza Prof. Busagala.

Kadhalika, aliwataka wasambazaji wa vyakula nchini kutumia Tume hiyo kupima vyakula ili kujihakikishia kuwa havina viasili vya mionzi hatari kwa afya za watumiaji.

Hata hivyo, Balozi Naimi Aziz, alisema lengo la ziara yake ni kujionea shughuli ambazo zinatekelezwa na Tume hiyo nchini.

"Kutokana na makao makuu ya shirika la kimataifa la Nguvu za Atomu duniani kuwepo nchini Austria katika mji wa Viena na mimi ndiyo kituo changu cha kazi nimeamua nije hapa ili nijifunze kile mnachofanya lakini pia kuangalia vipaumbele na changamoto zenu ili kuweza kuzisemea," alisema Balozi Aziz.




Balozi wa Tanzania nchini Austria, Naimi Aziz (kushoto), akizungumza na wafanyakazi wa Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania, Kikombo jijini Dodoma jana. Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Prof. Lazaro Busagala (katikati) na Mkurugenzi wa kitengo cha udhibiti wa mionzi cha tume hiyo, Dk. Justine Ngaila. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wananchi waazimia kumshtaki DC wao kwa RC

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

WAKAZI wa kijiji cha Mlowa B, wilayani Chamwino mkoani Dodoma, wamelalamikia kauli za vitisho kutoka kwa Mkuu wao wa wilaya, Gift Msuya na kuazimia kwenda kumshtaki kwa Mkuu wa Mkoa Rosemary Senyamule.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara wa kijiji hicho, mmoja wa wakazi hao Michael Samatwa, alisema mkuu huyo wa wilaya aliwatamkia hadharani kuwa, ubishi wa watu wa Mlowa kama ni nchi zingine walitakiwa kupigwa risasi.

Samatwa, alisema wakazi wa kikijiji hicho walijibiwa kauli hiyo baada ya kuhoji kuhusu mradi wa maji walio uendesha tangu mwanzoni mwa miaka ya 1970 wao wenyewe ambao hivi sasa wanashangaa kuona unakabidhishwa kwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Alisema mbele ya wananchi Mwenyekiti huyo wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa wilaya alitaka kila anachokisema kisihojiwe badala yake watu watekeleze.

"Ni kweli vijana walipaza sauti wakihoji kwa nini wanataka kuingiziwa watu wa RUWASA, ambao wanajifunza katika maeneo mengine wamefeli kwa hiyo kutaka kuwapa Mamlaka kwenye huduma hiyo ni kuwafanya wale fedha za kijiji chetu," alisema Samatwa.

Suzana Tupa, alisema amri ya Mkuu wa wilaya iliwapa mashaka kuwa wanakwenda kunyang'anywa mradi huo ambao tangu ulipoanzishwa na utawala wa awamu ya kwanza umekuwa ukiendelea vema na wananchi wanapata huduma ya maji.

Tupa, alisema kauli ya mkuu wa wilaya iliwandoa kwenye matumaini na kuwafanya waishi kwa hofu kwani wanajifunza katika maeneo mengine ambayo miradi yao walipewa RUWASA, lakini ikakwama.

Diwani wa Kata ya Mlowa, Anjelo Lukas, alisema hakuna kauli mbaya iliyotolewa na Mkuu wa wilaya siku ya mkutano isipokuwa kulikuwa na vijana waliokuwa wanapiga kelele wakati mkuu huyo akitoa ufafanuzi kuhusu miradi ya maji.

Lukas alisema kilichozungumzwa na Mkuu wa wilaya kuwa alisema Tanzania ni nchi ya kidemokrasi, lakini ingekuwa nchini zingine wanaopiga kelele kama hao wangeshughulikiwa ingawa hawezi kuwafanyia hivyo kwa sababu ya demokrasia iliyotamalaki.

Kuhusu mradi wa maji, Diwani alikiri lazima uchukuliwe na RUWASA kutokana na matumizi mabaya ya maji kijijini hapo ambao yanasababisha upotevu wa mapato huku baadhi ya wajanja wanachukua maji na kumwagia bustani zao bila kulipa wakati mitaa mingine wananchi hawana maji.

Hata hivyo, Gift alikanusha kutoa kauli hiyo mbele ya mkutano akisema hawezi kuwaambia Watanzania anaowaongoza maneno hayo ingawa kwenye suala la maji alisimamia sheria inayosema kila miradi ya uendeshaji wa maji kwa sasa itakuwa chini ya RUWASA.

Msuya alisema kauli zinazotolewa dhidi yake zinalenga kupotosha ukweli halisi kwenye miradi ambayo ni lazima wasimame kuwasaidia wananchi kwa kuwa kumekuwa na sintofahamu hasa katika uendeshaji wake.



## Polisi yajipanga matukio kushambuliwa watalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limesema limejipanga zaidi kukabiliana na uhalifu ikiwamo matukio ya kushambuliwa kwa watalii baada ya kuongezewa nguvu ya gari za kufanya doria.

Hayo yalisemwa na Kamishna wa jeshi la Polisi Zanzibar Hamad Khamis Hamad, wakati akikabidhi magari mawili yaliyotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya kufanya doria na kuimarisha ulinzi katika ukanda wa Wilaya ya Kusini Unguja.

Alisema magari hayo yametolewa ikiwa ni sehemu ya ahadi ya Rais Samia akiwa Amiri Jeshi Mkuu wa majeshi yote ya ulinzi na usalama katika mikakati ya kudhibiti uhalifu.

Kamishna huyo alisema matukio ya uhalifu kwa wageni ikiwamo utalii ni hatari na yanayoweza kurudisha nyuma mikakati ya serikali katika kuimarisha sekta hiyo na kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini.

Aliwataka watendaji wa jeshi hilo kujipanga zaidi kuhakikisha hakuna matukio ya uhalifu dhidi ya watalii na kufanya kazi kwa pamoja kwa kushirikiana na kikosi cha polisi utalii ambacho kipo kwa ajili ya kudhibiti matukio hayo.

"Jeshi la Polisi limekabidhiwa gari mbili hizi kwa ajili ya kufanya shughuli za doria katika ukanda wa utalii wa Mkoa wa Kusini Unguja ambapo matarajio yangu makubwa kwamba tutazitumiya vizuri kwa malengo yaliyokusudiwa kukabiliana na uhalifu," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, alisema hali ya usalama wa watalii katika ukanda huo ni nzuri na kwa zaidi ya miaka miwili hakuna matukio ya kushambuliwa kwa watalii.

Alisema wanafanya kazi vizuri kwa kushirikiana na polisi utalii katika kufanya doria maeneo yote ya fukwe za Mkoa wa Kusini Unguja ambayo yanahusisha hoteli za kitalii katika ukanda huo.

# Taasisi za serikali zatakiwa kutumia wazalendo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAASISI za serikali na binafsi zimetakiwa kuwatumia wakadiriaji majenzi kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi mbalimbali ili kukamilisha kwa wakati pamoja na kuokoa gharama zisizo za lazima.

Mkurugenzi wa ujenzi wa viwanja vya ndege, Injinia Mwanahamisi Kitego, alisema hayo wakati akifungua mkutano wa 29 wa Taasisi ya Wakadiriaji Majenzi Nchini ambao umeenda sambamba na uchaguzi wa viongozi wa taasisi hiyo.

Alisema, ni vyema kwa taasisi ikawatumia wakadiriaji ili kuondoa changamoto ya kukamilika kwa miradi pamoja na gharama za uendeshaji wa miradi na kuokoa fedha za serikali.

Alisema taaluma ya wakadiriaji majengo ni muhimu na ni wajibu wa wataalamu hao kuwa na ubunifu kwa vile dunia inakwenda na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Alisema katika kufanikiwa katika fani hiyo ni lazima watalaamu hao kuwa na uono wa mbali wa kwenda kufanya kazi nje ya Tanzania ili kujijengea uwezo na umaarufu katika nchi mbalimbali.

Aidha, alisema serikali imekuwa na ukaribu mkubwa na watalaamu hao katika kushauri mambo mbalimbali ya kujenda taifa la Tanzania hasa katika miradi hata ya miundombinu.

Aliwataka wakadiriaji majengo kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya kazi hiyo kwa lengo la kuokoa fedha katika miradi mbalimbali ya serikali na binafsi.

Naye Rais wa Taasisi ya Wakadiriaji Majenzi Tanzania, TIQS, Benard Ndakidemi, alitaka serikali kutoa nafasi za ajira kwa Wakadiriaji Majenzi katika taasisi za serikali ili kutoa ushauri wa mikataba ya ujenzi wa miradi na kuongeza ufanisi.

Alisema iwapo Serikali ya Tanzania itakuwa na ushirikiano katika kujenga miradi ya maendeleo majengo yatakuwa bora, yatakamilika kwa wakati na kuondoa upotevu wa fedha za wananchi.

Alisema taasisi hiyo imepata mafanikio makubwa tangu kuanzishwa kwake wanachama wengi wanaojiunga na jumuiya yao licha ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali katika maeneo yao ya kazi.

Washirikia wa mkutano huo walisema iwapo watashirikishwa katika serikali juu ya kujenga miradi ya maendeleo majengo yatakuwa bora na kukamilika kwa wakati, lakini kwa sasa ushirikishwaji wao hauko mkubwa.

Benard Ndakidemi, alisema fani hiyo ina umuhimu mkubwa katika jamii na ipo haja kwa miradi ya maendeleo hasa majengo kabla ya kujengwa kuona wao wakadiriaji wa majengo wanafanya nini kwa maslahi ya taifa.

Alisema bado kuna changamoto kubwa katika kuwatambuwa na ushirikishwaji wao katika vyombo vya serikali wakati umefika sasa kuona wanashirikishwa katika miradi ya majengo kwa kuokoa fedha za umma.



Baadhi ya wavuvi wa Kijiji cha Chwaka, Mkoa wa Kusini Unguja, wakifanya ukarabati wa zana za uvuvi kijijini hapo mapema wiki hii, kwa ajili ya maandalizi ya kwenda baharini kuvua. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yadhamiria kuwaletea maendeleo wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Zanzibar imedhamiria kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Zanzibar kupitia sekta mbalimbali bila ya kujali tofauti ya aina yoyote.

Hemed aliyasema hayo wakati akizungumza na viongozi, wanachama wa CCM na wananchi wa Jimbo la Chake Chake, Pemba, alipokuwa akihitimisha ziara yake ya majimbo 50 ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Alisema dhamira ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kujenga Zanzibar katika nyanja zote kiuchumi, kisiasa na jamii ili wananchi wawe na mazingira mazuri yaliyo bora.

Hemed ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais, alisema kuwa serikali itahakikisha kiwanja cha michezo cha Tibirinzi kinajengwa kwa kisasa chenye hadhi ya kimataifa ili kuibua vipaji na kukuza michezo nchini.

Aidha, alisema malengo ya Rais Dk. Mwinyi ni kuufanya mji wa Chake Chake kuwa ni sura ya Kisiwa cha Pemba na kukamilika kwa bustani ya kupumzikia eneo la Mwanamashungu, ujenzi wa barabara kutoka Chake Chake hadi Wete pamoja na miundombinu ya taa za barabarani kutasaidia kuweka haiba nzuri ya mji huo.

Akizungumza kwa niaba ya Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Zawadi Suleiman, amempongeza Rais wa Zanzibar kwa kuendelea kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa kujenga miradi mingi ya maendeleo.

Aliwataka wananchi kuthamini juhudi zinazofanywa na viongozi kwa kulinda miradi hiyo ili idumu kwa muda mrefu na iweze kufaa kizazi cha sasa na baadaye.

Katika ziara yake, Hemed alikagua na kushiriki ujenzi katika matawi, Maskani na maeneo ya vitega uchumi ya CCM, amepokea taarifa za utendaji kila Jimbo, amepokea wanachama wapya na kutoka upinzani, pamoja na kuzungumza na viongozi, wanachama na wananchi kwa majimbo hayo.



## BURNA BOY

UKURASA 14

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI SEPTEMBA 2, 2023



# ZAIDI YA NYOTA
## Kipaji chake gumzo

MTOTO mwenye kipaji cha muziki Bamiungu Rode maarufu kama Founder Tz (14), huenda safari yake ya kuelekea katika mafanikio imeanza baada ya lebo ya Wasafi kuonyesha nia ya kumchukua.

Founder Tz amepata umaarufu kupitia mitandao ya kijamii, kiasi cha kuitwa nyota change inayong'aa kutoka magharibi, wakimaanisha mkoa wa Kigoma ambao uko magharibi mwa Tanzania.

Kimtazamo Founder Tz ni mtoto mwenye kipaji cha asili, hata sauti yake inaonyesha dhahiri atakuwa msanii mkubwa endapo atatunzwa na kufundishwa vyema.

Mmoja wa mameneja wa WCB, ambaye ni Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, Hamisi Taletale maarufu kama Babutale ameonyesha nia kukilea kipaji cha mtoto huyo kwa kuahidi kumsomesha na kumuendeleza kimuziki.

"Nimependa huyu dogo anavyoimba na kwakua tumeumbwa kuwainua wenzetu ninaahidi kumsomesha na kumsaidia kutoa EP yake ya nyimbo nne," amesema Babu Tale.

Amesema yeye ni sehemu ya jamii walioona kipaji cha mtoto huyo, lakini kama kuna wengine wana nia kama yake wanaweza kufanya hivyo.

"Lengo ni kumsaidia na kutimiza ndoto yake, kama wananiamini na kuona naweza kumsaidia basi waniachie kwa sababu kukuza kipaji kunatakiwa umakini na pasiwepo nguvu kutoka nje ili kumuharibu," amesisitiza.

Historia ya Founder Tz anaanzia katika kambi ya wakimbizi ya Nyarugusu mkoani Kigoma, huko ndiko alizaliwa na wazazi wanaotokea nchini DRC.

Kimsingi amekulia katika familia ya kimasikini ambayo ilimbidi kulala chumba kimoja pamoja na mama na ndugu zake watatu.

Maisha hayo hayakumfanya kukata tamaa, badala yake aliongeza bidiii na kipaji chake kilichomoza kama jua la asubuhi na sasa amekuwa gumzo.

Kwa sasa Founder Tz anatamba na kibao chake kinachoitwa 'Nitatokaje' ambacho kimeangaliwa na idadi kubwa katika mtandao wa You Tube.

BASI SAWA

## Upo Single yainogesha tena Zabron Singers

KUNDI la muziki la Zabron Singers, limeendelea kuonyesha ubabe katika nyimbo za Injili zenye kubeba ujumbe wa maisha ya kila siku baada ya kuachia singo kali inayoitwa 'Upo Single'.

Mwalimu wa kundi hilo lenye maskani yake Kahama mkoani Shinyanga, Japhet Zabron amesema wimbo huo ni mwendelezo wao wa tungo zinazoshibisha sherehe mbalimbali na harusi.

"Baada ya kufanya vizuri na wimbo wa Sweetie Sweetie, sasa tumekuja na Upo Single, tunamshukuru Mungu kwa kutupa kibali hicho unaweza kuona ndani ya wiki moja tu video ya wimbo huu imefikisha watazamaji milioni moja katika mtandao wa YouTube," amesema Japhet.



## Wako tayari, we olewa tu

IDADI kubwa ya Watanzania wameonekana kuridhia mwanamitindo na mwanamuziki wa Bongo Fleva, Hamisa Mobetto kufunga ndoa na mpenzi wake wa sasa Kevin Sowax.

Wiki hii Hamisa alikuwa gumzo la mjini baada ya kuonekana na Sowax wakila raha kitika mitaa mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam.

Katika kunogesha penzi hilo zito, alitoa ombi kwa mpenzi wake huyo kwamba yuko tayari kuwa mke wake.

Mashabiki wake walivamia kurasa yake ya Instagram wakimpongeza kwa hatua hiyo na kumruhusu kuolewa kwa kuwa wote wanaendana.






## VERO USITAKE WAPIGANE VIKUMBO

MREMBO anayepamba video za wanamuziki mbalimbali, Vera Sidika ametangaza nafasi iko wazi kwa mwanamume yoyote anayejiona anaweza kummiliki.

Vera ambaye ni mama wa watoto wawili alitoa tangazo hilo mara penzi lake na mzazi mwenzake Brown Mauzo kuvunjika.

Amesema si kila mwanaume atakayetuma maombi atakubaliwa, bali atatumia vigezo vyake na Yule atakayeibuka mshindi ndiye atafikiriwa kuziba pengo.



## Kumbatio la Harmonize lina kitu?

USIKU wa Agosti 30, kwenye Tamasha la Kizimkazi kulitokea tukio la kipekee baada ya wanamuziki wakubwa nchini Harmonize na Ali Kiba kukumbatiana hadharani.

Tukio hilo lililopelekea kuwa na hisia tofauti, lilitokea wakati Harmonize alipomvamia Ali Kiba wakati akifanya mahojiano na kuanza kumkumbatia huku akimpongeza.

Hata hivyo, baadhi ya watu wanadhani linaweza kujitokeza hivi karibuni.

Wasanii wote wawili hao wako katika bifu zito na Diamond Platnumz.

# NYIMBO 5 ZA 'MAHARAMIA'

**Na Adam Fungamwango**

TANGU miaka ya nyuma hadi leo hii inatafutwa dawa ya kumaliza uharamia kwenye muziki lakini imekuwa kazi ngumu.

Baadhi ya wanamuziki au wasanii hasa maarufu na wenye majina makubwa wamekuwa wakichukua kazi ya wanamuziki au wasanii chipukizi wasio na majina na kujipatia sifa na pesa nyingi huku waliozitunga wakiambulia ahadi tamu, vitisho au kudhihakiwa.

Haya mambo unayoyaona leo msanii chipukizi akikwambia ngoma fulani ni yangu lakini imeibiwa au kuchukuliwa na msanii fulani kwa ahadi fulani lakini imekuwa kinyume chake ilikuwepo tangu miaka ya nyuma.

Mfano wimbo wa 'Malaika' ni wa Mtanzania aliyekuwa nchini Kenya akifanya kazi ya gereji na muziki, Adam Salim miaka ya 1960, lakini 'ukahodhiwa' na Fadhili William raia ya Kenya, lakini pia wimbo wa 'Dereva Kombo' uliompatia sifa mwanamuziki wa Kenya Fundi Konde, haukuwa wake, ila aliuiba kwa Mkenya mwenza Paul Mwachupa.

Leo nitaziweka nyimbo zilizoimbwa na wanamuziki wa hapa Bongo, lakini zinachukuliwa na 'maharamia. kiasi cha kuleta sintofahamu.

**Dada Asha**

Wimbo huu ulitungwa na Shem Karenga miaka ya 1970, wakati akipigia bendi ya Tabora Jazz na ukavuma kwelikweli.

Hata hivyo mwanzoni mwa miaka ya 1990, ukarekodiwa na bendi ya Soukous Stars ya wanamuziki wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo iliyokuwa na kina Lokassa ya Mbongo, Yondo Sister, Shimita Lokomb Nzambi, Ngouma Lokito, Saladdin Ferreira, Ballou Canta, Lucian Bokilo na wengineo ukiwa kwenye albam na wimbo uliotwao 'Nairobi Night.'

Hakukuwa na makubaliano yoyote kati ya mtunzi na wanamuziki hao ambao walidai waliuchukua kwa haki zote kutoka nchini Kenya kwenye moja ya studio iliyokuwa na ina haki miliki ya wimbo huo.

**Vigelegele**

Kesi ni hiyo hiyo, wimbo huo ulikuwa moja ya nyimbo zilizo kwenye safu ya kibao cha 'Nairobi Night' cha Soukous Stars.

Ukweli ni kwamba 'vigelegele' ni wimbo uliopigwa na bendi ya Tanzania, Western Jazz ukarekodiwa mwaka 1973, maharamia wakauchukua pia.

**Roza**

Pia ilikuwa ni hivyo hivyo, ndani ya wimbo wa 'Nairobi Night' mlikuwa pia na wimbo wa 'Roza' uliofyatuliwa na Western Jazz mwaka huo huo wa 1973, nao ulichukuliwa kiharamia na wanamuziki hao wa Soukous Stars.

**Dezo Dezo**

Mtunzi halisi wa wimbo huu ni marehemu Freddie Ndala Kasheba. Alitunga na kuurekodi na bendi yake ya Zaita Musica mwanzoni mwa miaka ya 1990. Ni miaka ambayo mwanamuziki, Tshala Muana alifanya ziara nchini Tanzania. Alipoondoka kumbe alikuwa na lake moyoni. Akachukua wimbo wa 'Dezo Dezo' na kurekodi nchini Ufaransa bila idhini ya mwenyewe.

**Kokola**

Tshala Muana ambaye naye ni marehemu, aliiba nyimbo mbili ukiwemo huu wa Kokola uliimbwa kwa lugha ya Tshiluba. Nadhani aliupenda kwa sababu na yeye asilimia kubwa anaimba nyimbo kwa lugha hiyo. Kasheba ambaye na yeye ni Mkongomani aliyekuwa akifanya kazi nchini ndiye mtunzi wa wimbo huo. Kabla ya kifo chake alikuwa akifutilia sana malipo yake aliyoahidiwa kulipwa baada ya kushtaki. Haikujulikana kama hadi anafariki alikuwa amelipwa au la.

FILAMU

# Fimbo ya Babu: Hupati thawabu

**Na Adam Fungamwango**

UCHAWI ni dhana iliyo kwenye jamii zetu, hasa za kiafrika. Huamini kwamba kuna watu ambao wana uwezo wa kuwatesa kwa magonjwa watu wengine, au kuwapotezea uhai wao.

Na wapo baadhi ya watu kwenye jamii hupenda kujinasibisha hilo ili waogopwe na jamii, hivyo kuwafanya kuheshimiwa na kupewa kipaumbele kwa sababu ya kihofiwa na watu.

Dhana hii ipo kwenye filamu ya 'Kifimbo cha Babu.'

Imechezwa na wasanii Adili Idd, Dorah Martin, Salum Katembo, Peterson Izack, Jordan Nally, Mariam Twaha, Fatma Chambuso, Sada Sagalo, Salome Msilombo, Veronica Libangu, Nandy Kunemka, Said Chinga, na Judith Mushi.

Kwenye kijiji kimoja sehemu moja nchini, kuna mzee anaitwa Chigwaya. Huyu ana nguvu za kishirikina ambazo zinasababisha kutesa na kumaliza watu.

Anaanza kumuua mume wa Vero aitwaye Amosi. Kwenye msiba,Vero anamkunja nusu ya kumpiga mzee Chigwaya akimtuhumu kumuua mumewe.

Hilo linamkera mzee huyo na kuahidi naye atamuondoa duniani. Katika kuomba msamaha anasema ili asimtoe duniani basi amuoe ili awe mke wa pili. Vero anatakataa na inakuwa mwisho wake duniani.

Mzee Chigwaya anaendelea kuleta hofu kwenye kijiji kiasi cha kuwa na misiba kila siku karibuni kila nyumba.

Mkewe anamjia juu akimwambia aache mambo ya ulozi. Badala yake naye anageuzwa dumu la maji.

Hata hivyo tayari mke alikuwa ameshatoa siri ya kinachomfanya kuumiza watu. Ni fimbo anayokuwa nayo mkononi. Alikuwa ameshamwambia kijana mmoja aliomuona ni mwaminifu kijijini.

Hatimaye kazi inafanyika, anahadaiwa kuwa mgonjwa, sehemu alipofika akaombwa asaidie kubeba, wakati akijiandaa, mmoja akampora kifimbo chake, nguvu za uchawi zikatoweka papo hapo. Kijiji kikarejea kwenye hali yake ya zamani ya amani na furaha.





## Burna Boy kwa wali hatoki

MWANAMUZIKI maarufu wa Nigeria, Burna Boy amesifia chakula aina ya wali kutoka Ghana akielezea ni mtamu kuliko unaopikwa nchini mwake.

Wakati wa mahojiano na Complex US, Burna Boy alimwagia sifa chakula hicho ambacho ni mchanganyiko wa mchele nyanya, vitunguu, viungo na mbogamboga.

Ingawa mwazoni wakati akipewa sahani zenye wali kutaja asili yake alikosea kwa kutaja inaweza kuwa kutoka Kenya.



## 'Utukufu concert' kutikisa Uganda

Baada ya kufanya vizuri kwenye chati za muziki wa injili Afrika Mashariki na kati, stay wa muziki huo Jonathan Budju, anatarajia kutikisa nchini Uganda na tamasha lake la Utukufu.

Jonathan mwenye makazi yake nchini Canada, ameliambia BT kuwa tamasha hilo litafanyika jijini Kampala, Disemba 17, mwaka huu katika viwanja vya Sharing Youth Center huko Nsambya.

"Maandalizi yanaendelea vizuri hapo Kampala na ninaamini nitakwenda kumtukikia Mungu kwa ukubwa hili ni tamasha langu la kwanza Afrika baada ya kufanya vizuri na nyimbo kubwa kama vile Hosanna, Matthieu na Utukufu,"

Aidha Jonathan amekuwa akishughulika na utoaji wa misaada watu wenye uhitaji barani Afrika kupitia taasisi yake ya Jonathan Budju Foundation..


## Lupita amkumbuka Chadwick

MSANII maarufu wa filamu kutoka Kenya, Lupita Nyong'o amemwagia sifa rafiki yake, Chadwick Boseman katika kumbukumbu ya miaka mitatu tangu afariki dunia.

Lupita alimwandikia barua ya kipekee katika ukurasa wake wa Instagram, akisema taarifa za kifo cha Chadwick ilikuwa ya uchungu kwake.

Pia alichapisha picha isiyo na rangi ya mwigizaji huyo akitabasamu kwenye uwanja wa ndege huko Korea, iliyochukuliwa mnamo 2018.

"Miaka mitatu iliyopita leo, nilipata uchungu wa pekee kwa taarifa za kifo cha @ chadwickboseman. Mkanganyiko ulikuwa mkubwa sana hivi kwamba ilichukua miezi kuamini hisia za furaha tena. Hii ni picha niliyopiga kwenye filamu kwenye uwanja wa ndege tulipofika Korea Kusini mnamo 2018," ameandika





## Iyanya kweli kapatikana

MWIMBAJI kutoka Nigeria, Iyanya, amefichua kwamba alikaribia kumpoteza mpenzi wake wa sasa baada ya kuibuka tuhuma ya uhusiano wa kimapenzi na mwigizaji Yvonne Nelson.

Iyanya amesema kuwa baada ya kusambaa kwa tuhuma hizo mwanadada huyo alikuwa akimuuliza suala hilo na kutilia shaka kuhusu uchumba wao.

"Madai ya Yvonne Nelson ni ya kichaa, mambo hayo karibu yamenifanya nipoteze uhusiano wa sasa," amesema.

Itakumbukwa kuwa Yvonne Nelson katika kitabu chake cha 'I Am Not Yvonne Nelson' alisimulia jinsi alivyogundua mpenzi wake wa wakati huo, Iyanya, alikuwa akimlaghai na mwigizaji wa Nollywood, Tonto Dikeh.

## 2baba awachukia wadukuzi

NYOTA wa muziki wa Nigeria, Innocent Idibia, maarufu kama 2baba, amesema wadukuzi wa mitandao ya kijamii ni sawa na magaidi ambao wanawaumiza sana wasanii.

Amesema wadukuzi wanaweza kuwarudisha nyuma wasanii kutokana na kuweka vitu visivyofaa kwenye kurasa zao za mitandao ya kijamii.

"Ninapata kazi nyingi. Nilipata watu wengi wanaosema mambo mengi kuhusu mimi. Watu wamenikanyaga mara kadhaa kwenye mitandao ya kijamii na wakati mwingine huumiza. Wakati mwingine baadhi ya watu wanadukua kurasa zangu na kuandika takataka," amesema.



## Serikali yakerwa utoroshaji mifugo nje ya nchi

**Na Tumaini Mafie,**
ARUSHA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo, Dk. Daniel Mushi, amesema hafurahishwi na vitendo vinavyoendelea vya utoroshaji wa mifugo kwenda nje ya nchi, kupitia mpaka wa Namanga, Wilaya ya Longido, mkoani Arusha.

Aliagiza wilaya hiyo kujipanga na kuweka doria za kutosha mipakani ili kuzuia vitendo hivyo.

Dk. Mushi, alieleza masikitiko yake hayo jana, alipokuwa katika ziara kwenye mnada wa mifugo wa Meserani na kiwanda cha kuchakata nyama cha Elia Food.

"Kumekuwapo na uhaba mkubwa wa mifugo hapa nchini. Hivi sasa, tatizo hilo linasababisha kushuka kwa soko la mifugo kutokana na utoroshaji wa mifugo kwenda nje ya nchi; jambo ambalo linaikosesha serikali mapato.

"Nawaagiza viongozi wote wa Wilaya ya Longido, mkae pamoja na kuunda timu maalumu ya kufanya doria katika maeneo ya mipakani ili kudhibiti utoroshaji huo, ambao unafanywa na wafugaji kwa lengo la kutafuta soko nje ya nchi, kwa njia zisizo halali."

Aidha, aliagiza viongozi hao kukaa meza moja na viongozi wa mila (Alaigwanani) ili kuwaelimisha kisha na wao watoe elimu kwa jamii zao za kifugaji, kuhusu madhara ya utoroshaji wa mifugo.

Awali, wakurugenzi wenza wa Kiwanda cha Elia food Overseas Ltd, Shabbir Virjee na Irfhan Virjee, kwa nyakati tofauti walisema, hivi sasa wamepunguza uzalishaji kiwandani kutokana na upungufu wa mifugo ambayo mingi inapelekwa nchi jirani.

Irfhan, alisema kwa kipindi cha nyuma walikuwa wanachakata mbuzi na kondoo 4,000, kwa siku sawa na tani 50.

Kutokana na utoroshaji huo, hali hiyo imesababisha kiwanda chao kukosa soko la nje walipokuwa wameingia mkataba kwa ajili ya kuwapelekea nyama.



Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Olpiro wa jamii ya Wadatooga wanaoishi ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wakiwa wamepanga foleni katika ofisi ya Kata ya Eyasi jana, kwa ajili ya kujiandikisha ili kuhama kwa hiari kwenye eneo la hifadhi. **PICHA: ALLAN ISACK.**

## Nchi nne zaomba kujifunza huduma za posta nchini

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

NCHI nne za Umoja wa Posta Afrika (PAPU), zimewasilisha rasmi ombi maalum kwa Rais Samia Suluhu Hassan la kutaka kuja nchini kujifunza huduma za posta ili ujuzi huo ukatumike kwenye mataifa yao kuchochea ukuaji wa sekta hiyo barani Afrika. Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Macrice Mbodo, alisema nchi hizo ni Kenya, Burundi, Zimbambwe na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

"Majirani zetu hao tayari wameomba kuja kujifunza kuhusu huduma za posta. Nia yetu wote, tutoa huduma zinazofanana katika bara letu hili, ndio maana kila nchi inapata uzoefu wa nchi zingine.

...hata sisi yapo mambo hatuyafahamu wenzetu wametutangulia, lakini nasi tumepiga hatua kubwa kwenye uboreshaji wa miundombinu yetu. Katika mkutano huu, tunajadiliana kuona jinsi ya uboreshaji wa huduma za posta na kutatua matatizo tunayokutana nayo."

Alisema moja ya hatua iliyopigwa Tanzania kwa sasa, ni utumiaji wa simu za kiganjani katika uagizaji wa mizigo mbalimbali ndani na nje ya nchi na kuagiza chochote kwa kutumia teknolojia hiyo, bila usumbufu wala kupoteza muda.

Pia, alisema Shirika la Posta kama sekta haitakufa, hata zaidi ya miaka 100, kwa sababu watoa huduma wake wanaendelea kujipanga na kufanya mageuzi ya kutosha kwenye utoaji wa huduma ili kusaidia maendeleo katika Bara la Afrika.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema wamekua na mikutano mbalimbali kwa makundi tofauti mkoani Arusha ya watoa huduma wa sekta ya posta barani Afrika ili kubadilishana uzoefu kwa ajili ya kuboresha zaidi utoaji wa huduma zao.

"Lakini leo tutamalizia na kikao cha Mawaziri wa sekta ya posta kwenye bara letu hili na kumalizia na uzinduzi wa jengo la makao makuu ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU), utakaozinduliwa na Rais Samia Hassan Suluhu, leo Septemba 2," alisema.

Alisema, jengo hilo ambalo ni bora zaidi mkoani Arusha na ni moja ya kivutio kikubwa kwa wageni mbalimbali.

Nape, aliomba wananchi kujitokeza kuungana na Rais Samia, kwenye uzinduzi huo na kuonyesha ukarimu kwa wageni mbalimbali watakaofika mkoani humo.

## Bilal ataka Taasisi ya Nelson Mandela ipae kiutafiti

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MAKAMU wa Rais mstaafu, Dk. Mohamed Gharib Bilal, ameiagiza Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), kupaa zaidi katika anga za juu kwenye utafiti na teknolojia kwa maendeleo ya nchi.

Dk. Bilal, alikuwa akizungumza jana jijini hapa, wakati wa hafla ya kumsimika Mkuu mpya wa taasisi hiyo, Omari Issa na kumsimika Makamu Mkuu wa taasisi hiyo, Prof. Maulilio Kipangula.

Alisema kwa kuwa taasisi hiyo ni imara, anatamani kuiona ikipaa zaidi katika anga za juu katika utafiti, ubunifu na teknolojia, ambazo zitanufaisha Watanzania na nyanja za viwanda.

"Nasema haya yanawezekana kuipaisha zaidi taasisi hii, kwa sababu leo mnaniaga rasmi, baada ya kuwa Mkuu wa taasisi hii wa kwanza.

"Katika kipindi changu cha uongozi licha ya kuiongoza taasisi ikiwa changa na kwa vipindi viwili, nilifanya jitihada na nilifanikiwa kuivusha na sasa inajulikana zaidi ndani na nje ya nchi, ikiwamo Bara la Afrika na Dunia.

...Nimekuja hapa kwa sauti imara, lakini ninahamu ya kuona taasisi hii, inapiga hatua zaidi na najua mwenzangu Omari Issa ataiweka taasisi hii katika anga za juu zaidi."

Naye, Mkuu wa taasisi hiyo, Omari Issa, alimshukuru Dk. Bilal, kwa utumishi wake chuoni hapo, kwa kuwa uongozi wake umeleta mafanikio makubwa kutokana na juhudi zake binafsi, kama kaulimbiu: "Taaluma kwa maendeleo ya Viwanda".

Alisema katika uongozi wake, Dk. Bilal aliongeza idadi ya wanafunzi kutoka 83 na kufikia 1,468 kwa sasa, huku 466 wakiwa wanawake.

Pia, alisema ili kuhakikisha wanafunzi wa kike wanaongezeka tayari wapo katika hatua za ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike na litachukua wanafunzi wanaonyonyesha na wajawazito.

Kaimu Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Prof. Lughano Kusikula, alimshukuru Dk. Bilal, kwa kuwa mkuu wa taasisi hiyo wa kwanza na awali taasisi hiyo ilikuwa changa, lakini ameipaisha na kujulikana ndani na nje ya nchi.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, alisema wizara ina matarajio makubwa kutoka kwa mkuu wa chuo mpya, ikiwamo kuongeza mchango wa sayansi na teknolojia katika kuchagiza maendeleo ya nchi.

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Vifo vya wachezaji wa timu ya taifa ya Zambia vilivyowaliza Wabongo

-Hadi leo hawajawasahau Chikwalakwala, Ndumba Mwila

**Na Adam Fungamwango**



Kikosi cha wachezaji wa timu ya taifa ya Zambia ambacho kiliteketea kwenye ajali ndege mwaka 1993 nchini Gabon kikienda kucheza na timu ya taifa ya Senegal. Aliyebaki hai hapo ni Kalusha Bwalya wa pili kutoka kushoto waliosimama ambaye hakuwemo kwenye ndege, kwani alitoka Uholanzi na kuunganisha moja kwa moja Dakar.

HADI leo hii, mashabiki walioanza kulifuatilia soka la Tanzania miaka ya 1980 na 1990 hawajaisahau timu ya taifa ya Zambia iliyopata ajali ya ndege katika Pwani ya Libreville nchini Gabon 1993 na kuua watu wote 30 waliokuwemo, ikiwa ni pamoja na wachezaji 18 wa kikosi hicho.

Ilikuwa ni huzuni kubwa kwa mashabiki wa soka na Watanzania wote pale ilipotangazwa kuwa wachezaji 18 wa timu ya taifa ya Zambia wamefariki dunia kwa ajali ya ndege iliyotokea jioni Aprili 27.

Wachezaji hao walikuwa wakielekea Dakar, Senegal kwa ajili ya mchezo wa kufuzu kucheza kombe la dunia dhidi ya timu ya taifa ya Senegal.

Wachezaji hao walikuwa wanakwenda kusaka tiketi ili nchi yao icheze Kombe la Dunia mwaka 1994 lililochezwa nchini Marekani na Brazil kutwaa ubingwa huo ikiifunga Italy kwa mikwaju 3-2 ya penati baada ya kutoka suluhu.

Kwa nini waliokufa kwenye ajali hiyo ni wachezaji wa timu ya taifa ya Zambia na waliohuzunishwa na kusikitishwa badala ya Wazambia wenyewe ni Watanzania?

Ni kwa sababu miezi mitano tu iliyopita walikuwa nchini Tanzania kucheza Kombe la Challenge wakati huo timu za Ukanda wa Kusini nao walikuwa kishiriki michuano hiyo inayoandaliwa na CECAFA.

Timu ya taifa ya Zambia ilikuwa kwenye kituo cha Mwanza pamoja na timu ya Tanzania Bara, pamoja na timu za Malawi, Ethiopia na Zanzibar, huku kituo cha Arusha kukiwa na timu ya kikosi cha pili cha Tanzania Bara kilichojulikana kama Kakakuona.

Kundi A ambalo lilikuwa Arusha, lilikuwa likicheza mechi zake Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha na Kundi B ambalo lilikuwa na timu hiyo ya Zambia lilichezea mechi zake CCM Kirumba.

Bingwa wa michuano hiyo alikuwa Uganda akimfunga Tanzania Bara bao 1-0 kwenye fainali, Zambia ikishika nafasi ya nne kwa kuitwanga Malawi mabao 4-0 yaliyofungwa na Kelvin Mutale na Patrick Banda ambao wote walifariki kwa ajali hiyo baadaye.

Wabongo wengi walikoshwa na soka lao, ukiacha mastraika wao, mawinga wao Moses Chikwalakwala na Numba Mwila walitoa fora kiasi cha kuacha majina hayo na vijana kuanza kujipachika mitaani.

Baada ya kumalizika mechi yao dhidi ya Malawi, kwa kutambua kuwa walikuwa kivutio jijini Mwanza, wachezaji wa timu ya taifa ya Zambia walizunguka uwanja mzima kuwapungia mashabiki waliojitokeza. Kumbe ndiyo walikuwa wanawaaga.

Siku ya tukio kikosi cha wachezaji 18 wa Zambia, benchi la ufundi na wafanyakazi wa ndege, walisafiri na ndege ya Zambian Air Force de Havilland Canada DHC-5D Buffalo iliyokuwa na usajili namba AF-319, kwa ajili ya mechi hiyo.

Uchunguzi uliofanyika baada ya ajali hiyo ulibaini kuwa rubani wa ndege hiyo alikuwa mchovu, lakini pia alizima mashine ya ndege hiyo baada ya kushika moto.

Wachezaji walioangamia katika ajali hiyo ni golikipa Efford Chabala, mabeki John Soko, Whiteson Changwe, Robert Watiyakeni, Eston Mulenga, kiungo wa kati Derby Makinka, mawinga Moses Chikwalakwala na Ndumba Mwila, na Wisdom Mumba, washambuliaji, Kelvin Timothy Mwitwa, Richard Mwanza, Samuel Chomba, Moses Masuwa, Kenan Simambe Godfrey Kangwa, Winter Mumba na Patrick Banda.

Waliopona katika kikosi hicho ni wachezaji wawili pekee nao ni nahodha wa timu hiyo wakati huo Kalusha Bwalya na Charles Musonda.

Bwalya alipanga kwenda moja kwa moja Senegal akitokea kwenye klabu aliyokuwa akichezea wakati huo, PSV Eindhoven ya Uholanzi bila kurejea Zambia, huku Musonda aliyekuwa akichezea klabu ya Anderlecht ya Ubelgiji akikosa kujiunga kutokana na majeraha.

Ulikuwa ni msiba mkubwa Afrika kwa wachezaji hao walizikwa kwenye Uwanja wa Mpira wa Miguu, ambao unajulikana Uwanja wa Mashujaa uliopo Lusaka, Zambia.

Miaka 19 baadaye timu ya taifa ya Zambia ilifanikiwa kutwaa Kombe la AFCON nchini Gabon, kwenye ardhi ambayo wenzao walifia, wakiitwanga Ivory Coast iliyokuwa na Didier Drogba kwenye mechi ya fainali kwa mikwaju wa penalti 8-7.

Kabla ya fainali, wachezaji na viongozi wa timu hiyo walikwenda eneo la Pwani ya bahari ambapo wenzao walipata ajali na kuweka mashada ya maua.

**Tuma meseji 0716 350534**



Mabaki ya ndege ya Zambian Air Force de Havilland Canada DHC-5D Buffalo yenye na usajili namba AF-319 ikiwa Pwani ya Gabon baada ya kuanguka na kuua watu 30 wakiwemo wachezaji 18 wa timu ya taifa ya Zambia.



Safu ya makaburi ya wachezaji wa timu ya taifa ya Zambia waliozikwa kwenye Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Mashujaa Lusaka inavyoonekana. Mwanamama huyu yupo kwenye kaburi la aliyekuwa kipa wa timu hiyo, Efford Chabala.

# Hofu ya mapinduzi Cameroon, viongozi wa jeshi watimuliwa

**YAUNDE,** CAMEROON

KIONGOZI mkongwe barani, Paul Biya wa Cameroon, amebadilisha safu ya uongozi wa jeshi lake siku moja baada ya mapinduzi yaliyotokea nchini Gabon. Rais Biya amefanya mabadiliko makubwa katika Wizara ya Ulinzi ya nchi yake na vikosi vya jeshi kwa kuwateua wakuu wapya.

Haijatolewa sababu kuhusu hatua hiyo.

Kanali Cyrille Guemo, ambaye ni mkurugenzi wa mawasiliano katika wizara ya ulinzi ya Cameroon, ameliambia shirika la habari la Uturuki kwamba uteuzi huo mpya ulikuwa kwenye meza ya rais kwa siku nyingi.

Lakini kutokana na upepo wa mapinduzi ya kijeshi ambao unaenea katika makoloni ya zamani ya Ufaransa, viongozi ambao wamekuwa madarakani kwa muda mrefu wameanza kuwa na wasiwasi. Ingawa mwanzoni urais wa Biya ulitishiwa wakati wanajeshi walipojaribu kunyakua mamlaka baada ya uchaguzi wake wa kwanza, tangu wakati huo alifaulu kudumisha uaminifu wa jeshi.

Hata hivyo, uteuzi huo mpya wa kijeshi unaelezwa hauna nguvu wa kuzia uwezekano wa kufanyika mapinduzi.

**BBC**

# Upinzani Zimbabwe kuandamana

**HARARE,** ZIMBABWE

CHAMA kikuu cha upinzani nchini Zimbabwe kimeitisha maandamano ya kitaifa na kutoa mwito wa kurudiwa kwa uchaguzi ambao kinadai uligubikwa na udanganyifu uliomrejesha mamlakani Rais Emmerson Mnangagwa.

Mwito huo kutoka kwa chama cha Citizens Coalition for Change (CCC) ulitolewa siku moja baada ya Rais Mnangagwa kusema uchaguzi ulikuwa halali na kuonya hatua kali itachukuliwa kwa yoyote atakayesababisha ghasia.

Maandamano hayo yamepanga kufanyika katika majimbo 10 nchini humo, huku chama hicho kikiwaomba wanaharakati kuanzisha kampeni za mitandaoni na kusambaza ushahidi wa udanganyifu uliofanyikwa kwenye uchaguzi huo.

CCC kina siku saba za kuwasilisha madai ya kupinga matokeo hayo ya uchaguzi mahakamani tangu tume ya uchaguzi ilipotangaza rasmi.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Zimbabwe ilimtangaza Mnangagwa kushinda uchaguzi kwa asilimia karibu 53 na mpinzani wake Nelson Chamisa wa CCC akipata asilimia 44.

**DW**

# AU yasitisha uanachama Gabon

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

UMOJA wa Afrika umesitisha uanachama wa Gabon na kupiga marufuku shughuli zake zote ndani ya chombo hicho kufuatia mapinduzi ya kijeshi.

Uamuzi huo umekuja baada ya kikao cha Baraza la Amani na Usalama la umoja huo kilichofanyika juzi.

Hapo awali, serikali ya Gabon ilisema itaingia katika kipindi cha mpito baada ya kuondolewa madarakani Rais Ali Bongo na kikosi cha walinzi wake.

Wanajeshi hao hawakutoa maelezo juu ya muda gani wataongoza kabla ya kurudisha mamlaka kwa raia.

Muungano wa upinzani umewataka viongozi wa kijeshi kujadili njia bora zaidi ya kusonga mbele.

Katika taarifa yao iliwataka raia wa Gabon kushukuru jeshi kuwa kuondoa ukoo wa Bongo.

Muungano huo pia ulishutumu jeshi kwa kutoonyesha dalili zozote kwamba wanapanga kurudisha madaraka kwa serikali ya kiraia.

Msemaji wa muungano huo, Alexandra Pangha, aliambia kipindi cha Newsday cha BBC, kuwa itakuwa upuuzi kwa wafuasi hao kumuapisha rais siku ya Jumatatu kabla ya taasisi walizozivunja kuzirudisha.

Alikosoa kusita kwao kufanya mazungumzo na chama chao ambacho alidai kilishinda uchaguzi wa urais uliofanyika Jumamosi iliyopita.

"Kufikia leo (jana) tumekuwa tukisubiri mwaliko kutoka kwa wanajeshi ili watueleze mpango wao ni upi," alisema Pangha.

Aliongeza kuwa haamini kwamba nasaba ya Bongo kama imeondoka mamlakani. Alidai, bila kutoa ushahidi, kwamba kiongozi wa mapinduzi, Jenerali Brice Oligui Nguema, alikuwa akiungwa mkono na wanafamilia wa rais huyo aliyepinduliwa.

**BBC**

# Ecowas yalegeza msimamo Niger

**ABUJA,** NIGERIA

RAIS wa Nigeria Bola Tinubu, ambaye ni mkuu wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), amependekeza kuwepo na kipindi cha mpito cha miezi tisa katika mchakato wa kurudisha demokrasia nchini Niger.

Pendekezo hilo ni la kwanza la na jumuiya ya ECOWAS tangu wanajeshi wa Niger walipoipindua serikali Julai 26, mwaka huu.

Jumuiya hiyo ya kikanda ilitoa tamko la kuivamia nchi hiyo kijeshi na kuiwekea vikwazo baada ya wanajeshi kumuondoa madarakani Rais Mohamed Bazoum.

Tishio la kupeleka kikosi cha kijeshi lilitolewa baada ya kukwama kwa mazungumzo ya kurejesha utawala wa kiraia.

Tinubu alisema hakutakuwa na msamaha wa kuviondoa vikwazo vilivyowekwa na ECOWAS hadi serikali ya Niger ifanye marekebisho chanya.

Kupinduliwa kwa serikali ya Niger kumezua wasiwasi katika nchi za Afrika Magharibi tangu mwaka 2020 wakati serikali za Mali, Guinea na Burkina Faso zimepinduliwa na wanajeshi.

Hofu imeongezeka zaidi kutokana na uasi wa jeshi nchini Gabon na kusababisha Rais Ali Bongo, kupinduliwa muda mfupi baada ya kutangazwa mshindi wa uchaguzi mwishoni mwa juma lililopita.

**DW**



Rais wa Burkina faso, Ibrahim Traore, akisalimiana na Naibu Waziri wa Ulinzi wa Russia Yunus-bek Yevkurov, katika Ikulu ya nchi hiyo jana. **PICHA: BBC**

# Burkina Faso, Russia wajadili ushirikiano

**OUAGADOUGOU,** BURKINA FASO

RAIS wa mpito wa Burkina Faso, Ibrahim Traoré amefanya mazungumzo na ujumbe wa Russia kuhusu ushirikiano wa kijeshi Ofisi ya rais wa nchi hiyo ilisema ziara hiyo iliyoongozwa na Naibu Waziri wa Ulinzi wa Russia, Yunus-bek Yevkurov, ilikuwa kufuatilia makubaliano yaliyofikiwa na Traoré na Rais Vladimir Putin katika mkutano wa kilele wa Russia na Afrika uliofanyika mjini St Petersburg mwezi Julai. Mazungumzo hayo yalilenga masuala ya usaidizi wa kijeshi ikiwa ni pamoja na mafunzo ya kijeshi, maofisa wa ngazi zote na marubani. Taarifa hiyo ilisema kulikuwa na mijadala kuhusu maeneo ya ushirikiano wa kiuchumi na nishati ya nyuklia. Ziara hiyo imefanyika wakati Russia ikitaka kuongeza juhudi katika ushawishi wa kisiasa na kiuchumi barani Afrika.

Kundi la mamluki la Urusi Wagner, ambalo kiongozi wake Yevgeny Prigozhin alifariki katika ajali ya ndege wiki iliyopita, lilikuwa likitaka kupanua shughuli zake hadi Burkina Faso.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**REHEMA ALLY HAMADY** anatangaza kupotelewa na cheti cha darasa la saba chenye namba PS **2003163-029** kilichotolewa na Shule ya Msingi **LANG'ATANDOIYE** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/6657/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TRYPHONE BURERWA RWEYEMAMU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 737 CDP** aina ya **Toyota Corona.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/RB/1071/2023.**

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MBEYA LILILOPO MBEYA**

**MAOMBI NA.95 YA MWAKA 2021**

**JAY GODWIN PETER KABISA::::::: MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**IS-HAAQ ABDULHAMID SULEIMAN::: MJIBU MAOMBI**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA : IS-HAAQ ABDULHAMID SULEIMAN**

Fahamu kwamba JAY GODWIN PETER KABISA amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 04/09/2023 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere mwenyekiti wa baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya Mjini.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 30/09/2023.

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**30/09/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**KITUO CHA KIHONDA PC**
**WILAYA YA MOROGORO MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**SHAURI LA MADAI/NDOA Na......08/2022**

**JINA LA MDAI: ELIZABETH RAPHAEL KAZIMOTO**

**JINA LA MDAIWA: MUGANDA MICHAEL**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu za madai katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa Elizabeth Raphael kazimoto wa Tubuyu Morogoro Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba(Eleza hapa habari za Madai). **MADAI YA PINGAMIZI YA KUKAMATA MALI KUTOKA KWA MDENI.** Kwa hiyo unatakaiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 08 mwezi 09 mwaka 2023 saa 3:00 Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo vielezo vyote vinavyohusu shauri hii kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 30 Mwezi 08 Mwaka 2023.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**

**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......11/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: EDWARD ELIYA MGINA wa FOREST**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA ENELISA ANDENGULILE MBWILE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 29 Mwezi 09 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 18 mwezi 08 mwaka 2023

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YEFTHA ISACK MATHAYO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 357 AMQ** aina ya **ISUZU TXD.** Chassis namba **1685939.** Engine namba **866108T337AMQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/1059/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAMAL AHMED ABEDI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 833 BAQ** aina ya Mitsubishi Pajero. Chassis namba **H57A0106874.** Engine namba **4A31EXTH5SA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/LOAN/1078/2023.**

---

**THE UNITED REPUPLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENT ACT**
**(CAP. 117 R . E 2019)**
**DEED POLL CHANGE OF NAME**

BY THIS DEED I, ATHUMANI ALLY MPONZI , of P.O Box 50, Cell **0764185731,** KIDATU , KILOMBERO, MOROGORO -TANZANIA, a natural born Tanzania citizen DO HERE BY wholly, absoluty and uterly renounces, relinquish and abondons the use of my former names ATHUMANI ALLY and ATHUMANI ALLY MPONZI adopt as from the date of this ded poll and in subsstituition for the name ATHUMANOI ALLY MPONZI.
For the purpose of evidence of such determination , I HEREBY DECLARE that I shall at all times hereinafter in records deed , decoments and other writings and in all actions upon all proceedings as well as in all Public and Pruivate dealings and transactions and crreations upon all whatsoever use and sign in the name of ATHUMANI ALLY MPONZI as my name in liue of ATHUMANI ALLY. I FURTHER STATE that the reasons for such change my names ATHUMANI ALPLY which rerorded in PSSSF File No. 42500 the surname 'MPONZI' is mistakenly and in NMB with Account number 21710044049 Middle name 'ALI' which is not correct , while the correct names is ' ALLY as Middle name and MPONZI as surname." So it's differ from my other documents such as in my National Identification Authority (NIDA) with registration Number 19610512674020000121 I register with name ATHUMANI ALLY MPONZI so I diceded to use the name ATHUMANI ALLY MPONZI as its appear in my National Identofication Authority and in my birth Birth Certtificate so as to have the uniformity of names in all documents which concerns me.
ANDI HEREBY authporize and request all people to designate and address me by thew adopted name of ATHUMANI ALLY MPONZI only.
IN WITNESS WHEREOF I, hereunder signed in rthe assumed name **ATHUMANI ALLY MPONZI** in the day in the manner hereinaftre appearing.

SIGNED and DELIVERED at Morogoro by the said ATHUMANI ALLY MPONZI ... 2023

BEFORE ME:

COMMISSIONER FOR OATHS

DEPONENT



---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 325 LA 2021**

**LEONARD S. NDESHAU......MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JOSEPH J. MAKIPONYA............MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**JOSEPH J. MAKIPONYA – POPOTE ULIPO/MLIPO**

LEONARD S. NDESHAU amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni(Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 5/9/2023 saa TATU asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 01 Mwezi 09, 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA KILOSA**
**S.L.P.29,KILOSA**

**YAH: MAOMBI MADOGO NA.99/2022**

**SALUMU A BAKARI (Usimamizi wa mirathi ya marehemu Bakari Budy)...MLETA MAOMBI.**

**VERSUS**

**1. ASHA MAULID........................................MJIBU MAOMBI**
**2. KABANGO GENERAL, BUSINESS CO LTD.....MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA KABANGO GENERAL, BUSINESS CO LTD**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Barazala Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kilosa,tarehe 05/09/2023 wewe binafsi au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kusikizizwa.Endapo haudhuria,Maombi yataitwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.

Imesainiwa leo tarehe 28 mwezi 08 Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
KILOSA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**M/S JAH PEOPLE INVESTMENT TRANSPORT LTD** inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 960 BCL** aina ya SCANIA. CHASSIS NO **01234234.** ENGINE NO. **4120043.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MKO/RB/2614/2023.**


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

Nipashe MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa pembezoni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa bianadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

# MAITI KWENYE KIROBA-20

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Ilionekana kuwa kazi imekamilika. Tessy ameuawa na mumewe Charton kwa sababu ya wivu wa mapenzi. Na mwanaume ambaye anadaiwa kuwa naye ni Barton ambaye mpaka sasa hajulikani alipo.

Angeweza kumwambia Inspekta Frank atangaze rasmi kuwa muuaji au wauaji wa Tessy wamepatikana. Ni watu wawili akiwemo mumewe Charton. Lakini hakutaka kufanya haraka kiasi hicho.

Eddy anaomba namba za wapenzi wa Charton. Nia yake hasa ni nini?

"Enhee, mlipochukua mzigo wa maiti na kumbebesha Mboneka Fisimaji mliupeleka wapi?"

"Tulienda nao mpaka Magomeni Mikumi. Pale tulichofanya ni kubadilisha gari tu kwa sababu za kiusalama. Tulimuacha Mboneka na yule dereva taxi waondoke, tukakodisha gari nyingine mpaka Kinondoni."

"Halafu?" Akauliza Eddy.

"Ilikuwa ni Kinondoni Biafra, tulipofika pale tuliwakuta vijana fulani wahuni. Tukawaita na kuwapa mzigo tukawaambia wakautupe popote pale na tukawalipa pesa. Wao sasa ndiyo wakawa wanajua wenyewe wapi waliupeleka."

Eddy ndipo alipofahamu kwa nini mabaki ya viungo vya Tessy yalionekana kwenye kiroba maeneo ya Kinondoni Msufuni.

Ni kwamba Tessy aliuawa Ukonga Banana. Maiti ikafungwa kama mali au mzigo kutoka huko mpaka Magomeni Mikumi. Halafu watu wakakodi tena gari hadi Kidondoni Biafra.

Alijua kabisa baada ya kuwakabidhi mzigo ule na kuwapa pesa vijana wa kihuni walitaka kujua kuna nini mle ndani. Walipokuta maiti nao ili kuepuka kukamatwa wakatafuta kiroba, wakamimina viungo vya marehemu na kwenda kuutupa sehemu nyingine ingawa hawakwenda mbali sana. Kinondoni Biafra na Msufini si mbali sana.

****************************

Akanyanyua simu na kumpigia Inspekta Frank.

"Niambie Eddy, mambo yanasemaje?"

"Nadhani tupo ukingoni kabisa."

"Nilipowaambia mabosi wangu kazi tukupe wewe nilikuwa namaanisha."

"Okay afande ni hivi. Nadhani kwa sasa mnamshikilia Mboneka Fisimaji."

"Ni kweli."

"Sasa huyu Tinga Patauli ndiye mmoja wa wauaji wa Tessy, nataka mje kumchukua na kumhifadhi."

"Du! Kazi nzuri sana, nadhani hili likiisha unaweza kunisaidia hata mimi kupandishwa cheo ndugu yangu, maana hata mabosi zangu suala hili limewaweka roho juu sana."

"Usijali rafiki yangu na mimi naomba iwe hivyo. Ila huyo Mboneka Fisimaji yeye alishiriki kubeba mzigo wa maiti, yeye atakuwa shahidi mzuri sana kwa sababu kuna kitu aliona."

"Okay Eddy."

"Mboneka hana hatia, ila anatakiwa kukaa ndani mpaka tutakapomtia mbaroni Charton Antony, ndipo aachiwe huru na awe anakuja kuripoti kila baada ya muda kwa sababu yeye ni msaada mkubwa kwenye ushahidi. Kwa sasa nacheweza kusema mwachieni kwani akitoka tu jamaa anaweza kujua kuwa anasakwa akatoroka."

"Ni kweli kabisa."

"Okay, nadhani wiki hii tunaweza kutangazia umma muuaji wa Tessy."

"Itakuwa safi sana Eddy, kazi nzuri nakutakia kila la kheri."

Katika mahojiano yake na mtuhumiwa Tinga Patauli pamoja na kupata baadhi ya vitu ambavyo vitaifanya kazi yake kukamilika, alivutiwa zaidi na wapenzi wa Charton, Nancy na Rukia.

Mpelelezi siku zote kazi yake ni kudhani, kuhisi na kuunganisha vitu kwa ajili ya kupata kitu sahihi au kitakachofanana kwa ajili ya kurahisisha upelelezi.

Kwa sababu Charton amemuua mkewe wa ndoa, hawa wanawake au wapenzi wake wanaweza kuwa na siri kidogo ambayo wanaijua ni kwa nini amefanya kitu hicho.

Na ndicho kitu pekee ambacho amebakisha Eddy ili kukamilisha kazi yake, pamoja na kwamba inasemekana aligundua kuwa ana mpenzi aitwaye Barton. Lakini hadi sasa kwa mujibu wa Tinga hawajawahi kumuona mtu huyo na wanahisi kuwa huenda amekimbia, amejificha au amejiua.

Tinga amekiri mbele yake kuwa ni kweli alimsaka kwa miezi miwili kwa ajili ya kummaliza hawajampata.

"Je ni kweli amejiua, au ameuawa? Inawezekana Tinga hasemi kweli kwenye hili," Eddy alijiambia.

Eddy akavutiwa zaidi kumpigia Nancy mpenzi wake wa zamani kuliko huyu mpya Rukia.

Aliona kuwa na Nancy ndiyo anaweza kufahamu vitu vingi kuliko mwenzake.

"Hallow hujambo?"

"Sijambo nani mwenzangu?" Sauti nyororo ya kike toka upande wa pili ikauliza.

"Mimi ni shemeji yako, rafiki yake Charton."




**Eddy akavutiwa zaidi kumpigia Nancy mpenzi wake wa zamani kuliko huyu mpya Rukia.**

"Nani Chimozi au Sungururuma?"

"Chimozi." Akajibu haraka haraka huku akikenua meno baada ya kuona hakufanya kazi kubwa sana kujitambulisha kama alivyotarajia.

"Una habari kwamba rafiki yangu tumeshazinguana nimeachana naye?" Mwanamke huyo aliendelea kufunguka kwenye simu bila kujua kuwa anayeongea naye siye aliyekusudiwa.

"He, shemeji kwa nini tena?"

"Hivi kweli ni rafiki yangu ni mtu wa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Rukia kweli? Yule msichana mbaya muuaji..."

"Muuaji?" Akadakia.

"Kwani we hujui, unataka turudierudie, mimi siwezi kusema maana najua kwenye simu si vizuri kuongeaongea hovyo, unaweza kujikuta unaambiwa ukatoe ushahidi bure, Kumbe shemeji nimeamini kikulacho ni nguoni mwako."

Alichogundua Eddy ni kwamba Nancy ana vitu vingi kifuani ambavyo vinaweza kumfanya apate kitu kingine ambacho hajakijua kwenye kesi hii.

Ana uhakika kuwa Charton ndiye aliyemuua mkewe akishirikiana na Tinga, hivyo kwa hili akawa anajiuliza Rukia naye kamuua nani?

"Kwani shemeji upo wapi saa hizi?"

"Nipo kwetu Boko."

"Basi tunaweza kuonana jioni?"

"Wapi, maana unanijua mimi, sikai sehemu bila mbili baridi."

Ndipo Eddy alipogudua kuwa Nancy ni mnywaji, hivyo ilikuwa rahisi tu kwake kumwambia akodishe bajaj mpaka Mwenge na kama atawahi kabla yake afike kwenye baa iliyo nyuma ya majengo ya TRA na kuagiza kinywaji yeye atafika baadaye.

"Basi shemeji kwanza nirushie hiyo pesa ya bajaj maana hapa sina hata mbuni."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# TIGO PESA MBUNGI CUP 2023 KUINUA BODABODA

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam (CMPD) kimeandaa mashindano ya mpira wa miguu yanayofahamika kama "Tigo Pesa Mbungi ya Bodaboda 2023", imefahamika.

**CMPD imeandaa mashindano hayo kwa kushirikiana na Kampuni ya Tigo, Car & General, EFM pamoja na Dk. Mwaka ForePlan International.**

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mashindano hayo, Juma Kinshashu, ambaye ni Mwakilishi wa mgeni rasmi Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema bodaboda wanapaswa kubadilika kwa kufanya kazi kisasa pamoja na kutumia fursa.

"Michezo ni afya, michezo ni ajira, ninawapongeza CMPD, serikali inaunga mkono jitahada zozote za michezo, ninawapongeza katika hilo, kupitia Tigo, jambo hili linaenda kuinua hali zenu kiuchumi, sasa mnapaswa kuthamini kazi zenu, mjue mnaenda wapi, lazima mwonyeshe mnabadilika na kuwa wa kisasa, tujijenge upya," alisema Kinshashu.

Naye Mwenyekiti wa CMPD, Michael Massawe alisema sekta ya bodaboda ina fursa nyingi za kiuchumi, hivyo ni muhimu kuwaunganisha na kuwaonyesha jinsi ya kuchangamkia na kunufaika na fursa hizo.

Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha alisema kupitia mashindano haya madereva pikipiki watapata fursa ya kujifunza njia mpya ya malipo kwa ajili ya kuongeza kipato chao.

"Tigo tumeona ni vyema kutumia nafasi hii ya kuwakutanisha bodaboda kwa ajili ya kuwapa fursa za kiuchumi, tutakuwa na nafasi ya kuwasaidia madereva pikipiki kutambua namna mpya ya kufanya malipo kupitia "Lipa kwa Simu" ambapo wateja wanaweza kulipa kwa simu zao za mkononi ili bodaboda waweze kupata pesa kupitia njia ya kidijitali" alisema Pesha.

Meneja wa Malipo ya Wafanyabiashara wa Tigo Pesa, Edgar Mapande, aliongeza;

"Ushirikiano huu na CMPD una manufaa makubwa kiuchumi yatakayosaidia madereva wa bodaboda kutimiza baadhi ya malengo yao, ikiwa ni pamoja na kunufaika na faida za uchumi wa kidijitali."

Mashindano hayo yanatarajia kushirikisha timu 64 kutoka katika wilaya tano za Dar es Salaam.




Mwenyekiti wa Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam (CMPD), Michael Massawe (aliyesimama), akizungumza katika uzinduzi wa mashindano ya Tigo Pesa Mbungi yatakayohusisha waendesha bodaboda yaliyofanyika jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Kipa wa Mazembe atua Coastal*

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuimarisha kikosi chake, uongozi wa Coastal Union inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara umetangaza rasmi kumsajili golikipa wa zamani wa mabingwa wa Afrika, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Ley Matampi.

Ofisa Habari wa Coastal Union, Abbas El Sabri, aliliambia gazeti hili Mkongomani huyo amepewa mkataba wa miaka miwili na wamemsajili akitokea klabu ya Renaissance ya DRC.

Mbali na Matampi, Coastal Union pia imemnasa beki wa kati, Konare Malienne, kutoka Mali ambaye wanaamini ataongeza nguvu katika kikosi chao.

"Tumekamilisha usajili wa Matampi kutoka DRC, na mchezaji mwingine raia wa Mali, lakini pia wakati dirisha linakaribia kufungwa (juzi) tulikamilisha usajili wa wachezaji wawili Watanzania ambao tutawatangaza," alisema Sabri.

Matampi, ameshawahi kuitumikia Timu ya Taifa ya DRC na kuzichezea klabu za AS Vita kati ya mwaka 2004 hadi 2005, DC Motema Pembe (2005 - 2012), TP Mazembe (2012 - 2014) na akaichezea tena 2016 -2018.

Nje ya DRC, kipa huyo amewahi kuitumikia Kabuscorp ya Angola na Al Ansar ya Saudi Arabia.



## Mbeya City, Green Warriors hapatoshi

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya City itakutana na Maafande wa Green Warriors katika mechi ya kufungua dimba katika Ligi ya Championship itakayochezwa Septemba 9, mwaka huu.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Bodi ya Ligi, mechi hiyo itachezwa Uwanja CCM Sokoine jijini Mbeya.

Ratiba hiyo inaonyesha Polisi Tanzania itakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, mkoani Mtwara kucheza dhidi ya Mbeya Kwanza ambayo imeamua kuchezea mechi zake katika uwanja huo.

Wakati wageni hao kwenye ligi ya Champioship wakikaribishwa na wenyeji, timu mbili ngeni ambazo zimepanda daraja, TMA na Stand United zitapambana zenyewe siku hiyo hiyo kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha huku kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Copco itawakaribisha Pan African ya Dar es Salaam.

Septemba 10, mwaka huu Fountain Gate itavaana na Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Jamhuri ,Morogoro huku KenGold ikiwaalika Transit Camp ya Dar es Salaam na Mbuni FC watakuwa wenyeji wa Biashara United.

## Majiha ajiimarisha kumpiga Mfipilino

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Fadhili Majiha, ameingia kambini kwa ajili ya kupigana na Renz Rosia kutoka Ufilipino katika pambano la 'Royal Tour Boxing Kanda ya Ziwa' litakalofanyika Septemba 30, mwaka huu jijini, Mwanza.

Akizungumza na Nipashe jana, Majiha alisema ameanza maandalizi ya pambano hilo mapema kwa lengo la kuhakikisha anafanya vizuri kama sehemu ya kuunga mkono juhudi za Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan, za kutangaza utalii wa ndani.

Majiha alisema amefurahi kupata pambano hilo kubwa la kimataifa ambalo litatangaza utalii wa ndani, kupitia mchezo wa ngumi.

"Tunaenda Mwanza kufanya mambo mawili muhimu, kutangaza utalii pamoja na kumchapa mpinzani wangu ili kuubakisha mkanda wa ubingwa wa ABU hapa Tanzania," alisema Majiha.

Naye promota wa pambano hilo, Hassan Kumbucha, alisema lengo la kuandaa mtanange huo ni kutangaza utalii pamoja na kuhamasisha mchezo huo katika Kanda ya

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**SALAH KUVUNJA REKODI**

KLABU ya Saudi Pro League Al-Ittihad iko tayari kutoa ada ya rekodi ya Ligi Kuu England ya pauni milioni 150 kwa Liverpool kwa ajili ya kumnasa mshambuliaji wa Misri, Mohamed Salah, mwenye umri wa miaka 31. (***Telegraph***)

**SPURS YAMTAKA JOHNSON**

KLABU ya Tottenham Hotspur itaangalia zaidi mpango wa kumnunua fowadi wa Nottingham Forest na Wales, Brennan Johnson, mwenye umri wa miaka 22, baada ya kushindwa na Brighton katika kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Barcelona na Hispania, Ansu Fati (20). (***Standard***)

**GALLAGHER ATAJWA SPURS**

TOTTENHAM Hotspur pia wanatathmini dau la kuchelewa la uhamisho wa kiungo wa kati wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 23. (***Telegraph***)

**FULHAM YAIBANIA BAYERN**

FULHAM wamekataa ofa ya awali kutoka kwa Bayern Munich kwa kiungo wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Palhinha, mwenye umri wa miaka 28. (***90min***)

**FULHAM, UNITED ZATETA**

KLABU ya Fulham imewasiliana na Manchester United kuhusu uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay, mwenye umri wa miaka 26. (***Sky Sports***)

**HOJBJERG SOKONI ENGLAND**

KIUNGO wa kati wa Tottenham Hotspur na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 28, pia anatazamwa kama chaguo linalowezekana kuchukua nafasi ya Palhinha, ambaye Fulham inamthamini kwa pauni milioni 60. (***Standard***)

**CHALOBAH NDOTO IMEPOTEA**

BAYERN Munich wameachana na mazungumzo na Chelsea kuhusu Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 24, baada ya The Blues kukataa kupunguza bei yao ya pauni milioni 50 ili kumnunua beki huyo wa kati wa England. (***90min***)

**AMRABAT ANUKIA UNITED**

MANCHESTER United wamepiga hatua katika mpango wa kumnunua kwa mkopo kiungo wa Fiorentina na Timu ya Taifa ya Morocco mwenye umri wa miaka 27, Sofyan Amrabat. (***90min***)

**BAKAYOKO KUTUA EPL**

BRENTFORD imewasilisha dau la rekodi ya klabu la pauni milioni 34 kwa PSV Eindhoven kuhusu fowadi wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Johan Bakayoko, mwenye umri wa miaka 20. (***90min***)

**SPURS: DIER HAONDOKI**

TOTTENHAM Hotspur imekataa ofa kutoka kwa Burnley kwa ajili ya mlinzi wa Timu ya Taifa ya England, Eric Dier, mwenye umri wa miaka 29. (***Football Insider***)

**DAVIS KUTUA UDINESE**

MSHAMBULIAJI wa England, Keinan Davis, mwenye umri wa miaka 25 anakaribia kukamilisha uhamisho wa kudumu kutoka Aston Villa kwenda Udinese. (***Nicolo Schira***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOUTHGATE: STERLING HANA FURAHA KUTEMWA ENGLAND

**LONDON,** England

**Kocha huyo amweleza hakutaka kupangua kikosi chake ambacho...**

KOCHA, Gareth Southgate, amekiri Raheem Sterling "hana furaha kabisa" baada ya kuachwa katika kikosi cha timu ya taifa ya England.

Sterling mwenye umri wa miaka 28 ni mmoja wa wachezaji wenye uzoefu mkubwa na timu ya taifa lakini hajaongeza mchezo wowote kwa timu hiyo tangu ile 82 alipocheza kwa mara ya mwisho Desemba, mwaka jana wakati wakitolewa katika hatua ya robo fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Ufaransa.

Sterling alikosa mechi ya England iliyochezwa Machi, mwaka huu kutokana na jeraha na tatizo la misuli ya paja lilipelekea kile ambacho kambi yake ilieleza kama "uamuzi wa pande zote mbili" wa kuzingatia kuuponya mwili wake baada ya msimu wa kwanza kule Chelsea.

Lakini fowadi huyo hakupokea wito aliotarajia baada ya kuanza vyema msimu huu, huku Southgate akimwacha kwa mechi ya kufuzu kwa Euro 2024 dhidi ya Ukraine itakayochezwa wiki ijayo na ile ya kirafiki kule Scotland.

"Tulifurahishwa sana na kikosi chetu Juni," alisema kocha huyo wa England.

"Ili kumrejesha Raheem ni lazima tumwache mtu mwingine nje na sikufikiri kuna mtu yoyote katika kundi hili la wachezaji washambuliaji anastahili kuachwa.

**"Ni vizuri sana kumwona akianza msimu vizuri sana. Anaonekana katika hali nzuri, anaonekana ana njaa.**

"Ni wazi ni mchezaji muhimu kwetu na amekuwa mchezaji muhimu.

"Lakini katika maeneo hayo ya ushambuliaji tuko nyuma tu ya zile tisa ushindani mkubwa wa nafasi.

"Nadhani wachezaji hao wote wameanza msimu vizuri na hakika kundi ambalo tuko pamoja nasi limefanya vyema kwa ajili yetu katika michezo ya hivi majuzi."

"Hakupatikana kwa mechi mbili zilizopita na bila shaka hiyo imewapa watu wengine nafasi ya kucheza vizuri na kujiimarisha kwenye kundi.

"Ni uteuzi mgumu na Raheem hajafurahishwa haswa kuhusu hilo, lakini ninaelewa hilo kwa sababu ni mchezaji muhimu kwetu.

"Nina hakika atakuwa na msimu mzuri na Chelsea, hakuna shaka juu ya hilo."

Southgate aliamua kumpigia simu Sterling kuhusu uamuzi wake kwani alijua kwamba amekuwa "mchezaji mkubwa sana kwetu" na alitaka kutambua jinsi amekuwa akicheza vizuri.

"Raheem huwa anaheshimu sana jinsi anavyojibu na kushughulikia mambo," aliongeza Southgate.

"Siku zote atasema 'tazama, naheshimu uamuzi wako' lakini bila shaka anataka kurejea kundini. Na sitarajii hivyo kwa njia nyingine yoyote."

Fowadi huyo ameanza mechi tatu za kwanza za Ligi Kuu England akiwa na Chelsea msimu huu, akifunga mara mbili na kutoa asisti katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Luton Ijumaa iliyopita.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,148,6

MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
FULLHAM
1 | 1.22
X | 6.53
2 | 12.69

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Emmanuel Kusaja - 0653 535 XXX
2. Bonifasi Mitula - 0655 877 XXX
3. Edward Yosia - 0676 945 XXX
4. Laila Malisi - 0677 850 XXX
5. Thomas Haule - 0678 679 XXX
6. Omar Daud - 0679 837 XXX
7. Arafa Ahmadi - 0710 457 XXX
8. Juma Mtaze - 0710 493 XXX
9. Saidi Kitumbi - 0711 227 XXX
10. Hadson Ngadia - 0719 949 XXX
20,000/=
KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# REGUILON ATUA MAN UNITED KWA MKOPO

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imesajili beki wa pembeni wa Tottenham Hotspur, Sergio Reguilon kwa mkopo.

United ilikuwa inatafuta beki wa kushoto, huku Luke Shaw na Tyrell Malacia wakiwa nje kwa muda mrefu kwa sababu ya majeruhi.

Mazungumzo na Chelsea kuhusu Marc Cucurella yalishindikana kufikia hitimisho chanya, lakini kuhusu Reguilon, raia wa Hispania mambo yakawa poa.

United pia ilijaribu kukamilisha dili la kumnunua mchezaji wa Fiorentina, Sofyan Amrabat, ambaye aliichezea Morocco katika Kombe la Dunia mwaka jana, yuko chini ya mkataba hadi 2024 na klabu hiyo ya Serie A.

Reguilon mwenye umri wa miaka 26, alifuzu vipimo vyake vya afya na huenda akajumuishwa kwenye kikosi cha Erik ten Hag kwa safari ya kuivaa Arsenal hapo kesho.

Beki huyo alijiunga na Tottenham kutoka Real Madrid Septemba, 2020 kwa mkataba wa miaka mitano, lakini alikaa kwa mkopo Atletico Madrid msimu uliopita.

# Newcastle yatupwa kundi la kifo UEFA



**NYON,** Uswisi

DROO ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2023-24 imefanyika na mabingwa watetezi, Manchester City wakiwekwa kundi moja na RB Leipzig, huku Newcastle wakipewa kibarua kigumu.

Kikosi cha Kocha, Pep Guardiola kiliishinda Inter Milan 1-0 mjini Istanbul Juni mwaka huu na kutwaa taji la kwanza la Ulaya tangu kunyakua Kombe la Washindi wa Kombe la Ulaya mwaka 1970.

Na sasa lazima watafute njia ya kuipita Leipzig tena, ambao waliishinda kwa jumla ya mabao 8-1 katika hatua ya mtoano msimu uliopita.

Mabingwa hao wataungana na Crvena Zvezda na Young Boys katika Kundi G ambalo linaoneakana mchekea kwa mabinga hao watetezi wa Ligi Kuu England.

Wakati huohuo, Newcastle wamewekwa kwenye kundi gumu na wamepangwa na Paris Saint-Germain, Borussia Dortmund na AC Milan kwenye kundi F.

Kwingineko, Harry Kane atakuwa akirejea England wakati Bayern Munich itakapomenyana na Manchester United katika Kundi A na nahodha huyo wa Simba Watatu pia atakipiga dhidi ya FC Copenhagen na Galatasaray.

Kurudi kwa Arsenal kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kumewaweka Kundi B ambapo watakutana na washindi wa Ligi ya Europa, Sevilla, PSV Eindhoven na Lens ya Ligue 1.

**MAKUNDI**

**Kundi A**
Bayern Munich, Manchester United, Copenhagen, Galatasaray

**Kundi B**
Sevilla, Arsenal, PSV Eindhoven, Lens

**Kundi C**
Napoli, Real Madrid, Braga, Union Berlin

**Kundi D**
Benfica, Inter Milan, FC Salzburg, Real Sociedad

**Kikundi E**
Feyenoord, Atletico Madrid, Lazio, Celtic

**Kundi F**
Paris Saint-Germain, Borussia Dortmund, AC Milan, Newcastle

**Kikundi G**
Manchester City, RB Leipzig, Crvena Zvezda, Young Boys

**Kundi H**
Barcelona, Porto, Shakhtar Donetsk, Royal Antwerp

## HABARI MICHEZO

# WABUNGE, WATUMISHI WA BUNGE 'KUONYESHANA KAZI'

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

BENKI ya NMB imetoa udhamini kwa Bunge Bonanza linalotarajiwa kufanyika leo jijini hapa pamoja na kutoa vifaa mbalimbali vya mazoezi venye gharama ya Sh. milioni 130.

Kati ya fedha hizo, Sh. milioni 90 zimetumika kununua traksuti na vifaa vinginevyo vya michezo vitakavyotumiwa na timu ya Bunge na watumishi wa chombo hicho watakaoshiriki michezo mbalimbali.

Michezo itakayochezwa katika bonanza hilo ni mpira wa miguu, kikapu, pete, riadha, kukimbiza kuku, kukimbia na mayai, kuvuta kamba, karata na bao.

Akizungumza jana baada ya kukabidhiwa vifaa hivyo, Mwenyekiti wa Bunge Bonanza ambaye pia ni Mbunge wa Makete, Festo Sanga, alisema bonanza hilo litafanyika kwenye Uwanja wa Shule ya John Merlin.

Alisema lengo la bonanza hilo ambalo limebebwa na kaulimbiu ya 'Tushiriki Michezo Jenga Jamii Yenye Afya', ni kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo kwa sasa serikali inakabiliana nayo.

Sanga alisema wanatamani kila bonanza wawe wanaongeza michezo kwa kuwa serikali imekuwa inahamasisha Watanzania kufanya mazoezi ili kujikinga na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Alisema kama Bunge wameona waweke miili yao sawa ili kupambana na magonjwa hayo.

Sanga alisema mgeni rasmi katika bonanza hilo atakuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, ambaye ataambatana na wabunge zaidi ya 10 kutoka visiwani huko.

Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Janeth Shango, alisema benki hiyo ina utamaduni wa kushirikiana na Bunge, ndiyo maana wametoa udhamini wa vifaa kwa ajili ya michezo hiyo.

Alisema lengo la michezo hiyo ni ili kuwa na taifa lenye watu wenye afya bora na wataendelea kufanya hivyo katika mabonanza yatakayofuata.

"Tuwaombe wabunge pamoja na wananchi kuendelea kuitumia benki hii kama ambavyo tumeendelea kuwa wamoja na sisi tunaahidi kuwa pamoja nanyi kwa kila jambo ili mradi tujenge nchi kwa kuwa na watu wenye afya njema," alisema.


Festo Sanga

## Al-Merrikh yavunja mapumziko Yanga

INATOKA UK 24

yaliyoko mbele yao.

"Hakuna sababu ya kupumzika, tulipumzika siku moja na tayari tumerejea uwanjani, tunatakiwa kufikia malengo yetu, hivyo ni vyema tukaongeza nguvu katika kipindi hiki kuhakikisha tunafikia tunapohitaji," alisema Gamondi.

Aliongeza Al-Merrikh ni timu nzuri ina wachezaji ambao wanaweza kupata matokeo, hivyo hakuna umuhimu wachezaji kupumzika wakati wanahitaji kucheza hatua ya makundi.

"Yanga haijawahi kufika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tunahitaji kutumia mapumziko ya Ligi Kuu kwa ajili ya kuendelea kutengeneza timu na kufanyia kazi makosa yaliyojitokeza katika mechi zilizopita, ikiwamo kuruhusu bao au kusababisha penalti," Gamondi alisema.

Yanga imesonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuwaondoa ASAS FC ya Djibouti kwa jumla ya mabao 7-1, michezo yote miwili ikichezwa kwenye Uwanja wa Azam, kufuatia wapinzani wao kutokuwa na uwanja wa nyumbani wenye viwango kwa sasa.

Msimu uliopita Yanga ilicheza fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya mabingwa USM Alger ya Algeria lakini ikakosa taji kwa faida ya mabao ya ugenini waliyofunga Waarabu hao.

Yanga ilifungwa mabao 2-1 hapa nyumbani na wakashinda goli 1-0 ugenini.

## *Simba SC yaongeza dozi kwa mastraika*

INATOKA UK 24

"Ule ulikuwa mchezo wa kirafiki, mchezo wa kirafiki na mchezo wa mashindano ni vitu viwili tofauti, tunaiangalia Power Dynamos katika jicho kali sana, tunakwenda na tahadhari zote," alisema kiongozi huyo.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema mashabiki wanaokwenda kuishangilia timu yao katika mechi hiyo ya ugenini wataondoka nchini Septemba 13, mwaka huu na utaratibu wa safari unatolewa katika ofisi ya klabu yao.

Ahmed alisema gharama za usafiri wa kwenda na kurudi kwa kila shabiki ni Sh. 200,000 na mwisho wa kupokea fedha hizo ni Septemba 10, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Simba inatarajia kucheza mechi ya kirafiki leo dhidi ya timu ambayo haijatangazwa huku pia ikijiandaa kuelekea Kenya kuweka kambi ya muda mfupi kabla ya kwenda Zambia.


43,241/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 02/09/2023 | 19:30 | Brighton & Hove Albion vs Newcastle United | 2.50 | 3.55 | 2.50 |
| 02. 02/09/2023 | 19:45 | Go Ahead Eagles vs SC Heerenveen | 2.60 | 3.60 | 2.39 |
| 03. 02/09/2023 | 20:00 | Portimonense SC vs Estrela Amadora | 2.60 | 3.15 | 2.65 |
| 04. 03/09/2023 | 14:00 | Glasgow Rangers vs Celtic Glasgow | 2.36 | 3.45 | 2.75 |
| 05. 03/09/2023 | 14:30 | KAA Gent vs Club Brugge | 2.32 | 3.55 | 2.70 |
| 06. 03/09/2023 | 15:00 | FC Andorra vs Tenerife CD | 2.19 | 3.00 | 3.45 |
| 07. 03/09/2023 | 16:00 | Kalmar FF vs Mjallby AIF | 2.25 | 3.00 | 2.90 |
| 08. 03/09/2023 | 17:00 | Union Saint-Gilloise vs Royal Antwerp FC | 2.31 | 3.35 | 2.85 |
| 09. 03/09/2023 | 17:15 | RCD Mallorca vs Athletic Bilbao | 3.00 | 3.00 | 2.40 |
| 10. 03/09/2023 | 17:30 | GD Chaves vs Moreirense FC | 2.29 | 3.20 | 3.05 |
| 11. 03/09/2023 | 17:30 | Estoril Praia vs Boavista Porto | 2.38 | 3.20 | 2.90 |
| 12. 03/09/2023 | 17:30 | FC Basel 1893 vs FC Zurich | 2.55 | 3.35 | 2.33 |
| 13. 03/09/2023 | 18:00 | Stroemsgodset IF vs Stabaek IF | 2.15 | 3.35 | 2.80 |
| 14. 03/09/2023 | 18:30 | IFK Norrkoping FK vs Djurgardens IF | 2.65 | 3.30 | 2.29 |
| 15. 03/09/2023 | 18:30 | Union Berlin vs RB Leipzig | 3.10 | 3.25 | 2.24 |
| 16. 03/09/2023 | 19:30 | KRC Genk vs RSC Anderlecht | 1.95 | 3.65 | 3.40 |
| 17. 03/09/2023 | 20:15 | Royal Charleroi SC vs St. Truidense VV | 2.17 | 3.35 | 3.10 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 02/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1776 | Magdeburg vs Hertha BSC | 2.26 | 3.75 | 2.70 |
| 14:00 | 3330 | Holstein Kiel vs Paderborn | 2.25 | 3.79 | 2.70 |
| 14:00 | 4087 | Wehen vs Schalke 04 | 3.09 | 3.59 | 2.09 |
| 14:30 | 1864 | Birmingham vs Millwall | 2.28 | 3.07 | 3.07 |
| 14:30 | 1911 | Sheffield Utd vs Everton | 2.94 | 3.19 | 2.52 |
| 14:30 | 4119 | Swansea vs Bristol City | 2.04 | 3.36 | 3.31 |
| 14:30 | 4630 | Sunderland vs Southampton | 2.67 | 3.47 | 2.34 |
| 15:00 | 4328 | Real Sociedad vs Granada | 1.49 | 4.44 | 6.60 |
| 16:30 | 1925 | Stuttgart vs SC Freiburg | 2.22 | 3.55 | 3.14 |
| 16:30 | 2287 | Augsburg vs VfL Bochum | 2.01 | 3.70 | 3.55 |
| 16:30 | 2712 | Hoffenheim vs VfL Wolfsburg | 2.53 | 3.65 | 2.62 |
| 16:30 | 5310 | Werder Bremen vs Mainz | 2.63 | 3.60 | 2.55 |
| 16:30 | 5914 | Bayer Leverkusen vs SV Darmstadt | 1.23 | 6.59 | 11.32 |
| 17:00 | 1353 | Brentford vs Bournemouth | 1.74 | 3.92 | 4.53 |
| 17:00 | 1407 | Burnley vs Tottenham | 3.70 | 3.90 | 1.91 |
| 17:00 | 1447 | Stoke City vs Preston | 1.90 | 3.36 | 3.76 |
| 17:00 | 1451 | West Bromwich vs Huddersfield | 1.68 | 3.71 | 4.45 |
| 17:00 | 1851 | Middlesbrough vs QPR | 1.58 | 3.92 | 4.96 |
| 17:00 | 2205 | Manchester City vs Fulham | 1.22 | 6.53 | 12.69 |
| 17:00 | 3188 | Coventry vs Watford | 2.10 | 3.36 | 3.17 |
| 17:00 | 3325 | Rotherham vs Norwich City | 4.07 | 3.72 | 1.74 |
| 17:00 | 3351 | Plymouth vs Blackburn | 2.58 | 3.58 | 2.36 |
| 17:00 | 3695 | Chelsea vs Nottingham | 1.45 | 4.61 | 6.91 |
| 17:00 | 4302 | Leeds vs Sheffield Wed | 1.42 | 4.37 | 6.36 |
| 17:00 | 5560 | Ipswich vs Cardiff | 1.62 | 3.86 | 4.65 |
| 17:15 | 2812 | Sporting Gijon vs Burgos | 2.02 | 3.03 | 3.77 |
| 17:15 | 3248 | Real Madrid vs Getafe | 1.38 | 4.65 | 8.92 |
| 17:30 | 1239 | U.Leiria vs Avs Futebol Sad | 2.13 | 3.17 | 3.22 |
| 17:30 | 1805 | Casa Pia Atletico vs Rio Ave | 2.10 | 3.33 | 3.24 |
| 17:30 | 3447 | Almere City vs PEC Zwolle | 3.03 | 3.52 | 2.10 |
| 17:30 | 3585 | Penafiel vs Viseu | 2.66 | 3.32 | 2.39 |
| 18:00 | 3381 | Brest vs Rennes | 3.30 | 3.60 | 2.13 |
| 19:15 | 1763 | Pendikspor vs Alanyaspor | 2.27 | 3.57 | 2.74 |
| 19:15 | 2784 | Basaksehir vs Konyaspor | 2.30 | 3.30 | 2.89 |
| 19:30 | 1241 | Alaves vs Valencia | 2.89 | 2.95 | 2.74 |
| 19:30 | 1530 | Bologna vs Cagliari | 1.71 | 3.80 | 4.93 |
| 19:30 | 2103 | Brighton vs Newcastle | 2.62 | 3.75 | 2.49 |
| 19:30 | 2526 | Udinese vs Frosinone | 1.83 | 3.66 | 4.33 |
| 19:30 | 4024 | Monchengladbach vs Bayern Munchen | 6.63 | 5.68 | 1.38 |
| 19:45 | 4038 | GO Ahead Eagles vs Heerenveen | 2.19 | 3.51 | 2.87 |
| 20:00 | 4219 | Maritimo vs Pacos Ferreira | 2.07 | 3.37 | 3.17 |
| 20:00 | 4877 | Portimonense vs CF Estrela | 2.59 | 3.13 | 2.64 |
| 20:00 | 5367 | Famalicao vs Sporting Farense | 1.76 | 3.53 | 4.28 |
| 21:45 | 3615 | Antalyaspor vs Kayserispor | 1.93 | 3.61 | 3.45 |
| 21:45 | 4240 | Atalanta vs Monza | 1.63 | 4.11 | 5.14 |
| 21:45 | 5154 | Napoli vs Lazio | 1.66 | 3.96 | 5.15 |
| 21:45 | 5655 | Gaziantep BB vs Galatasaray | 5.63 | 4.37 | 1.47 |
| 22:00 | 1526 | Heracles Almelo vs SBV Excelsior | 1.78 | 3.71 | 3.86 |
| 22:00 | 1614 | Monaco vs Lens | 2.09 | 3.80 | 3.23 |
| 22:00 | 2105 | Betis vs Rayo Vallecano | 2.00 | 3.45 | 3.86 |


CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Nipashe

Jumamosi Septemba 2, 2023

UK. 22




## Newcastle yatupwa kundi la kifo UEFA




Wachezaji wa Yanga, Stephanie Aziz Ki (kushoto), Maxi Nzengeli (katikati) na Hafiz Konkon wakishangilia baada ya timu yao kufunga bao katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya ASAS FC ya Djibouti iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

# Al-Merrikh yavunja mapumziko Yanga

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha timu yake haipoi, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameelekeza kikosi chake kiendelee na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kuwakabili wapinzani wao kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Al-Merrikh ya Sudan, imeelezwa.

Badala yake kocha huyo alitoa mapumziko ya siku moja na tayari wachezaji wa timu hiyo wameingia kambini kuendelea na maandalizi.

Yanga imeanza msimu huu kutoa vipigo vizito katika Ligi Kuu Bara pamoja na Ligi ya Mabingwa Afrika, michuano hiyo ikisimama kupisha kalenda ya kimataifa.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara watarejea tena dimbani ugenini Septemba 16, mwaka huu huko Sudan na mchezo wa marudiano utafanyika Septemba 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Taarifa kutoka ndani ya timu hiyo zinasema Gamondi amegomea wachezaji kwenda mapumziko katika kipindi hiki akisema wanaratiba ngumu mbele yao.

"Awali tulitarajia timu itakuwa na mapumziko, lakini Gamondi akasitisha, ametoa siku moja pekee ya kupumzika na baadaye amewataka wachezaji warejee kambini kuendelea na programu kwa nyota wote ambao hawajaitwa katika vikosi vya timu za taifa, anataka kasi waliyokuwa nayo iendelee watakapoikabili Al-Merrikh," kilisema chanzo chetu.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema anaamini ana kikosi bora chenye uwezo wa kupata matokeo katika mchezo wowote lakini hataki kuona wachezaji wanaenda mapumziko kwa sasa kwa sababu ya mashindano

INAENDELEA UK 23

# SIMBA SC YAONGEZA DOZI KWA MASTRAIKA

## Robertinho atambulisha mbinu mpya huku Manula akirejea katika...

**Na Saada Akida**

WAKATI droo kwa ajili ya mashindano ya Afrika Super League inatarajia kufanyika leo usiku, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' ametambulisha mbinu mpya kwa wachezaji wake za kuhakikisha wanatumia vyema mipira ya krosi ili kufunga mabao kwenye michezo mbalimbali wanayocheza.

**Kwa sasa Simba inajiandaa na mchezo wake wa kwanza wa raundi ya pili ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos utakaochezwa Septemba 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa ulioko katika mji wa Ndola, Zambia.**

Simba ambayo imeanza msimu huu kwa kubeba Ngao ya Jamii mbele ya watani zao Yanga, itachuana katika kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mashindano ya Kombe la FA.

Nipashe ilifika katika mazoezi ya Simba jana asubuhi na kushuhudia Robertinho akiwataka wachezaji warudie mara kwa mara zoezi hilo ambalo anaamini likifanikiwa, litasaidia katika kuongeza nguvu na hatimaye timu kufikia malengo.

Mbrazil huyo jana alitumia saa mbili kwa ajili ya kukiona kikosi cha timu hiyo kwa kufanyia pia kazi mipira ya faulo na alifurahishwa kuona makipa wake, Ally Salim na Hussein Abel, wakiwa makini kudaka mipira kwenye zoezi hilo.

Pia Nipashe lilimshuhudia kipa chaguo la kwanza la timu hiyo, Aishi Manula 'Tanzania One' akianza programu maalum ya mazoezi kwa ajili ya kurejea langoni.

Manula alikuwa akifanya mazoezi binafsi chini ya uangalizi wa daktari wa timu hiyo, Edwin Kagabo.

Baada ya mazoezi kumalizika, Robertinho alisema licha ya safu yake ya ushambuliaji kuendelea kufunga katika kila mchezo, bado anawataka kuona wachezaji wa timu hiyo wanaongeza juhudi kwa kutumia vizuri mipira ya krosi ili kupachika mabao.

Kocha huyo alisema timu yake inaendelea kuimarika siku hadi siku licha ya baadhi ya wachezaji wachache bado hawajafikia ubora anaohutaji lakini anaamini kabla ya kukutana na Power Dynamos watakuwa wameimarika.

"Mipango yetu ipo katika michuano iliyopo mbele yetu, tunaendelea na maandalizi kwa ajili ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika licha ya kuwakosa baadhi ya wachezaji ambao wamekwenda katika timu zao za taifa lakini hatuwezi kukaa bila ya kujiimarisha.

Kikubwa tupo katika wakati mzuri kwa sababu timu inapata matokeo ya ushindi wakati wote na inatengeneza nafasi, ingawa nataka kuona wakitumia vyema mipira ya krosi kufunga mabao ambayo yatatusaidia kupiga hatua kubwa na kupunguza presha ambayo itakuwa kwenye upande wetu, " alisema Robertinho.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again' ametamba sababu ya ufunguzi wa michuano ya Ligi ya Afrika unafanyika Tanzania kwa sababu timu yao ni kubwa.

Salim aliliambia gazeti hili mafanikio ambayo Simba imeyapata ndio yamewapa heshima na Tanzania kuteuliwa kuwa mwenyeji wa mechi ya ufunguzi.

"Simba ni kubwa, mashabiki wa Simba wanapenda mpira, Watanzania wanapenda mpira," Salim alisema.

Mwenyekiti huyo pia alisema kikosi chao kinajiandaa vyema na kitakwenda Zambia kucheza mechi dhidi ya Power Dynamos kwa tahadhari.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >